Nipashe
Alhamisi Machi 14, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579865
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Dereva Bajaj asakwa kwa kumgonga trafiki

UKURASA 3




UKURASA 13



# Pigo lingine kwa Mbowe

• **Serikali** yatangaza kutaifisha kiwanja chake, mwenyewe afunguka na kusema... *Ukurasa 2*

## Malori ya diwani yanaswa magendo

UKURASA 2



UKURASA 2

## UDSM kigugumizi rushwa ya ngono

MICHEZO **WAWA AWATULIZA SIMBA SC** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Magari ya diwani yanaswa na mbao, magogo

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, imekamata magari manne yakiwamo mawili yanayodaiwa kuwa ya Diwani wa Sabasabini, yakiwa na shehena ya mbao 1,000, nguzo na magogo madogo 244 yaliyovunwa kinyume cha sheria ya misitu kwenye mapori ya akiba ya serikali.

Ofisa Misitu wa Halmashauri hiyo, Tadeo Elias, alisema mbao zilizokamatwa ni za mninga na mkurungu pamoja na nguzo 244 zote zikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 17.

Alisema mbao hizo zimevunwa kinyume cha Sheria ya Misitu Na. 14 ambazo uvunaji wake lazima upate kibali kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kuzingatia kanuni na taratibu za sheria

INAENDLEA UK. 8



Rais John Magufuli akimwonyesha Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi, Mikhail Bogdanov, picha ya Mlima Kilimanjaro ambayo alimkabidhi kama zawadi kabla ya mazungumzo yao Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**


**KUMBUKUMBU**



ELISA GEORGE MALLYA

Leo ni miaka kumi tangu alipoungana na Bwana (14 Machi 2009). Tunamkumbuka sana kwa hekima, busara na upendo wake. Alikuwa zaidi ya baba na rafiki wa karibu. Alikuwa, amekuwa na ataendelea kuwa wa thamani kwetu. Ingawa ametuacha wakiwa; LAKINI kumbukumbu yake na sala tulizoshiriki pamoja zinatupa nguvu, faraja na ujasiri wa kuondokana na machungu ya kutokuwepo kwake. Tuna imani siku tutakapokutana pamoja itakuwa ni kicheko, amani na furaha milele.

Unakumbukwa na Mke wako Ester, watoto wako Fred, Lillian, Kleist, Stella, Corona, Justin, Clara, Albert, Dorris, Simbo na Selina. Aidha na wajukuu, ndugu na marafiki zako.

**Tunakumbuka faraja uliyotuachia kutoka 1 Wathesalonike 5:16 - 22 "…Furahini siku zote; Ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu. Msimzimishe Roho; msitweze unabii; jaribuni mambo yote; lishikeni lilo jema; jitengeni na ubaya wa kila namna…"**

115113302


# Pigo lingine kwa Mbowe

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SIKU chache baada ya kutoka mahabusu, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amekumbana na pigo lingine baada ya uongozi wa Wilaya ya Hai kutangaza nia ya kupoka kiwanja chake.

Jana, uongozi wa wilaya hiyo ulitangaza kuwa tayari umeshawasilisha kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ilani ya ubatilisho wa umiliki wa wamiliki 34 wa viwanja vilivyoko eneo la maendelezo ya viwanda la Weruweru wilayani Hai.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alidai wameamua kuchukua hatua hiyo kutokana na wamiliki wa viwanja hivyo kudaiwa kodi ya pango la ardhi.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, wamiliki hao wa viwanja 34, kwa pamoja wanadaiwa kodi ya pango la ardhi inayofikia Sh. 1,828,166,096.

Mbali na Mbowe, orodha ya wadaiwa hao iliyotolewa Ole Sabaya jana, pia ina majina ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Cynthia Ngoye, Kiwanda cha Kutengeneza Vipuri cha Kilimanjaro Mashine Tools Manufacturing Company Ltd kilichoko chini ya Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) na wafanyabiashara maarufu wa Mji wa Moshi wanaomiliki shule binafsi na kampuni za utalii.

Akitangaza orodha hiyo jana,

INAENDELEA UK. 8

# UDSM kigugumizi rushwa ya ngono

**Na Romana Mallya**

UONGOZI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), umesema unajiuliza maswali mawili kuhusu uchunguzi wa tuhuma za rushwa ya ngono zinazowakabili baadhi ya wahadhiri wake.

Tuhuma hizo ziliibuliwa mwishoni mwa mwaka jana na Mhadhiri Mwandamizi wa chuo hicho, Dk. Vicensia Shule, kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

Muda mfupi baada ya Rais John Magufuli kuwasili UDSM kuzindua maktaba ya kisasa, Dk. Shule aliandika maneno kwenye ukurasa wake huo akisema:

"Baba Magufuli JP, umeingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufungua maktaba ya kisasa. Rushwa ya ngono imekithiri mno UDSM. Nilitamani nikupokee kwa bango langu, ila ulinzi wako umenifanya ninyamaze. Nasubiri kusikia toka kwako maana naamini wateule wako ni waadilifu, watakwambia ukweli."

Kutokana na kuibuliwa kwa tuhuma hizo, uongozi wa UDSM

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

13-03-2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 21-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam** kuelekea **Ifakara,** gari hilo lenye namba za usajili:

**T 881 AUX / T 137 CHN**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 20 |
| **Upana** | - | mita | 3.20 |
| **Kimo** | - | mita | 4.80 |

3. **Njia itakayotumika:** Dar es salaam hadi Ifakara kupitia Mikumi, Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215115502



**WHITE STAR INVESTMENTS LTD**
**TRANSPORTER**

**MADEREVA WA MAGARI MAKUBWA WANAHITAJIKA HARAKA**

**SIFA: -** Awe na uzoefu wa miaka mitano na zaidi.
Awe na uwezo wa kuendesha magari ya SEMI/PULLING
Awe na leseni pamoja na
Hati ya kusafiria (Passport)

**Muhimu:** Fika ofisini kwa usaili Kiluvia Madukani.

**Mawasiliano: 0692 136160**
**0689 251512**

**Au email: whitestarmapambano@gmail.com**

115115202

## HABARI KITAIFA

# Dereva bajaji asakwa kwa kumgonga trafiki

**Na Marco Maduhu,**

SHINYANGA

DEREVA wa bajaji yenye namba za usajili MC 649 BVE ambaye hajafahamika jina, mkazi wa wilayani Kahama mkoani Shinyanga, anasakwa na polisi kwa tuhuma za kumgonga askari wa usalama barabarani, Jenipher Mgogo (25) na kumsababishia majeraha sehemu mbalimbali za mwili wake.

Tukio hilo lilitokea Machi 11, mwaka huu majira ya saa 9:00 jioni katika eneo la Mashineni barabara ya Kahama kwenda Kiiza, mkoani Tabora.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, alisema juzi kuwa trafiki huyo akiwa katika majukumu yake ya kusimamia sheria za usalama barabarani, ilitokea bajaji hiyo ikiwa katika mwendokasi na hatimaye kumgonga kisha dereva kukimbia.

Abwao ilisema trafiki huyo alipata majeraha kichwani, usoni na mikononi pamoja na abiria Andrew Msumba (29), Mkazi wa Kahama, alipata majeraha miguuni. Alisema wote walipelekwa hospitalini kwa matibabu.

**"Chanzo cha ajali hii ni dereva huyo wa Bajaji ambaye alikuwa akiendesha kwa mwendokasi huku akiwa amebeba abiria. Baada ya kumwona trafiki barabarani akimsimamisha, ndipo alimgonga na kuaguka wote chini. Baada ya hapo aliamka na kuitelekeza Bajaji hiyo na kukimbia...**

"Chanzo cha ajali hii ni dereva huyo wa Bajaji ambaye alikuwa akiendesha kwa mwendokasi huku akiwa amebeba abiria. Baada ya kumwona trafiki barabarani akimsimamisha, ndipo alimgonga na kuaguka wote chini. Baada ya hapo aliamka na kuitelekeza Bajaji hiyo na kukimbia kusikojulikana," alisema Abwao.

"Majeruhi hawa wote, abiria na askari wetu, walilazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa ajili ya kupatiwa matibabu na hali zao zinaendelea vizuri," aliongeza.

Kamanda Abwao alisema Jeshi la Polisi bado linamsaka dereva wa bajaji hiyo na kuwataka wananchi watoe ushirikiano ikiwa atafahamika na kwamba bajaji yake wanaishikilia kituoni.

# Maandalizi Siku ya Maji yanoga

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajia kuungana na mataifa mbalimbali kuadhimisha Siku ya Maji Duniani ambayo huadhimishwa Machi 22, kila mwaka.

Mwaka 1993, Umoja wa Mataifa (UN) kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira na Maendeleo lilipitisha azimio rasmi la kuadhimisha Siku ya Maji Duniani kila mwaka ifikapo tarehe hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Maji, lengo kuu la maadhimisho hayo nchini ni kuungana na mataifa mengine duniani katika kutathmini utekelezaji, mafanikio, changamoto na kuainisha mikakati ya kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira na kusimamia utunzaji wa rasilimali za maji.

Taarifa hiyo ilisema maadhimisho hayo yatakwenda sambamba na kaulimbiu ya Wiki ya Maji Duniani, 2019 inayosema: "Hakuna Atakayeachwa: Kuongeza Kasi ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa wote katika Dunia Inayobadilika Kitabia Nchi."

Ilisema miongoni mwa madhumuni ya siku hiyo ni kuelimisha jamii kuhusu sera ya maji na majukumu yao katika kuitekeleza, kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa Programu ya Maji.

Ilitaja lengo lingine kuwa ni kutathmini hali ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira nchini na kuweka mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Taarifa hiyo ilisema maeneo mengine yanayotiliwa mkazo ni kuwaleta pamoja wataalamu wa sekta ya maji katika majadiliano, kujifunza na kubadilishana uzoefu na kuhamasisha ubunifu wa kisayansi katika utafiti na teknolojia katika utoaji wa huduma na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Ilisema siku hiyo itatumiwa kutathmini mafanikio ya sekta ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, na pia kuwakutanisha wadau mbalimbali wa taasisi binafsi, wadau wa maendeleo na serikali. Ilisema siku hiyo itakuwa fursa kwa wadau hao kubaini fursa za uwekezaji kupitia sekta ya maji na kutathmini mchango wa sekta ya maji katika tasnia nzima ya maendeleo ya viwanda nchini.

Ilisema katika kuadhimisha Wiki ya Maji, Wizara ya Maji, inashirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya maji katika kutathmini utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira pamoja na uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

"Wiki hii inaenda sambamba na shughuli mbalimbali zinazohusiana na utoaji wa huduma ya maji na utunzaji wa vyanzo vya maji nchini," ilisema.

Aidha, taarifa hiyo ilisema Wiki ya Maji ni fursa maalum ya sekta ya maji nchini kujitathmini kwa kujilinganisha na nchi nyingine duniani katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya maji.


WIZARA YA MAJI

**Maadhimisho ya Wiki ya Maji Kitaifa yatafanyika jijini Dodoma kuanzia tarehe 18-22 Machi, 2019 katika ukumbi wa mikutano wa St. Gaspar.**

*Yatakayojiri ni;*
*Tarehe 18-19 Kongamano la Kisayansi Kuhusu Sekta ya Maji*

*Tarehe 20-21 Siku maalum ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ripoti ya utendaji wa mamlaka za maji ya mwaka 2017/2018 itazinduliwa na kujadiliwa.*

*Tarehe: 22 Kuhitimisha na mkutano wa mapitio ya hali ya sekta ya maji*

*Aidha, Tarehe 18-22 yatafanyika Maonesho kuhusu ubunifu katika huduma za sekta ya maji. Wadau wanakaribishwa kuonesha huduma hizo. Kwa maelezo zaidi wasiliana na wafuatao:*

*Vallentina Chaya: vallentina.chaya@maji.go.tz (+255 655 652 828)*

*Enock Wagala: enock.wagala@maji.go.tz (+255 716505627)*

*Maonesho yatakuwa wazi kwa wananchi, hivyo wote mnakaribishwa.*

*KAULIMBIU:*
*"Hakuna Atakayeachwa: Kuongeza Kasi ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Wote katika dunia inayobadilika kitabia nchi"*

*Limetolewa na:*
*Katibu Mkuu*
*Wizara ya Maji*

215106102



TANZANIA REVENUE AUTHORITY

**TAARIFA KWA UMMA**

**MABADILIKO YA TAREHE YA MWALIKO WA KIKAO KWA WASHAURI WA KODI (TAX CONSULTANTS)**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inawaalika Washauri wa Kodi **(Tax Consultants)** waliopo Jijini Dar es Salaam kwenye kikao kitakachofanyika siku ya **Jumatano tarehe 20/03/2019** kuanzia saa 3:00 asubuhi katika Ukumbi wa **KARIMJEE** uliopo **Jijini Dar es Salaam.**

Kikao hiki kimelenga kujadili changamoto na maboresho katika masuala ya ukusanyaji wa kodi ili kuinua ulipaji kodi wa hiari.

Kwa maelezo zaidi, piga simu bure: **0800780078 / 0800750075 AU Barua pepe Huduma@tra.go.tz** na pia unaweza kututumia ujumbe kwa njia ya **WhatsApp** kwenda namba **0744-233-333**

*"PAMOJA TUNAJENGA TAIFA LETU"*

215112302

# JPM, mjumbe wa Putin wateta Dar es Salaam

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alikutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Russia ulioongozwa na Mjumbe Maalum wa Rais wa nchi hiyo katika masuala ya Afrika na ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mikhail Bogdanov, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilisema Rais Magufuli alimshukuru Rais wa nchi hiyo, Vladimir Putin, kwa ushirikiano na uhusiano mzuri kati yake na Tanzania.

Pia alimhakikishia kuwa serikali anayoiongoza inatambua umuhimu wa uhusiano huo na kwamba itauendeleza na kuukuza zaidi hususani katika masuala ya biashara, uwekezaji, utalii na utoaji wa huduma za kijamii kama vile afya, elimu na miundombinu.

"Naomba ufikishe ujumbe wangu kwa Rais Putin kuwa Watanzania wanaipenda Urusi (Russia) na tunamkaribisha kuja kutembelea nchi yetu pamoja na wananchi wengine wa nchi hiyo. Tunawakaribisha pia wawekezaji waje wawekeza katika fursa mbalimbali zilizopo hapa Tanzania kwa manufaa yetu sote," alisema Rais Magufuli kama alivyokaririwa na taarifa hiyo.

Kwa upande wake, Bogdanov ambaye amewahi kutembelea Tanzania miaka minane iliyopita, aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kasi nzuri ya maendeleo iliyoyapata katika kipindi kifupi na alibainisha kuwa Russia imedhamiria kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati yake na Tanzania.

Bogdanov alisema nchi yake ina mpango mahususi wa kushirikiana na nchi za Afrika ikiwamo Tanzania katika kuongeza kasi ya maendeleo na kwamba hivi karibu Tanzania na nchi hiyo zitatiliana saini makubaliano ya kuanzisha tume ya pamoja ya ushirikiano katika biashara, uwekezaji

INAENDELEA UK. 8


IFAD Investing in rural people

FARM RADIO INTERNATIONAL

**CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST**

**Terminal Evaluation of Up-scaling of Interactive Information and Communication Technologies to Increase Uptake of Agricultural Innovations in Tanzania (UPTAKE) Project**

**1.0 Background**

Farm Radio International (FRI) is a Canadian non-profit organization that is at the forefront of using radio combined with other ICTs to serve smallholder farmers. The **Up-scaling of interactive information and communication technologies to increase uptake of agricultural innovations in Tanzania** (UPTAKE) project is funded by IFAD and contributes to the overall New Alliance Programme for Food Security and Nutrition under its Information and Communications Technology (ICT) Extension Challenge Fund. The project is implemented in collaboration with CABI.

The specific goal of the project is to contribute to increased agricultural production and productivity by scaling up the use of productivity-enhancing agricultural innovations and marketing mechanisms by small-scale farmers, using a combination of ICT-enabled agriculture extension approaches (participatory radio, mobile services), integrated and engaging with traditional extension services and linking to IFAD's existing programmes.

**2.0 Evaluation objectives and questions**

The primary objective of the terminal evaluation is to assess the achievement of objectives of the UPTAKE project. It will also identify and document lessons learned, and provide concrete recommendations for improving the performances of UPTAKE consortium members in future interventions.

**3.0 Scope of the Assignment**

The terminal evaluation will be conducted in the Pwani, Tanga, Njombe, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro, Arusha and Iringa regions of the United Republic of Tanzania. These are the areas in which the UPTAKE project was implemented. The evaluation will focus on synthesizing evidence of the relevance, effectiveness, efficiency, impact, and sustainability of the project, and on lessons learned, based on information collected from farmers, broadcasters, project staff, knowledge partners, and input supply partners.

**4.0 The Consultancy Team and Required Qualifications**

The competing firms for this assignment should be **"NATIONAL CONSULTANTS"** and possess the following competencies and qualifications.

- The evaluation team should be composed of a communication for development (C4D) and/or ICT for development (ICT4D) expert, agricultural extension expert, a social scientist, and a statistician.
- Extensive and dependable experience, skill and knowledge of conducting surveys, interviews, participatory methodologies, and data analysis (qualitative and quantitative).
- Experience evaluating communication for development projects (preferably rural and agricultural development) is mandatory.

**5.0 Proposal Submission**

- Bidders should submit renewed trade licenses, tax certificates, professional licenses, and other required documentation as indicated in the instruction to bidders.
- Bidders should submit their technical and financial proposals electronically at the following address: tanzania@farmradio.org
- The deadline for submission of proposal is **March 20, 2019.**
- No bid documents submitted after the specified deadline will be accepted.
- Incomplete applications will be disqualified.

*Any inquiries about the comprehensive ToR should be addressed to rchapota@farmradio.org*

215114901


## Hasunga awatangazia vita wauza mbegu feki

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amewatangazia kiama wafanyabiashara wanaouza mbegu na viuatilifu feki na kusema watu hao ni maadui wanaotakiwa kuchukuliwa hatua kali.

Hasunga alisema jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) Kanda ya Afrika, Prof. Shaukat Abdulrazak.

Katika mkutano huo uliotuama kwa saa kadhaa ulifanyika kwenye ukumbi wa Wizara ya Kilimo jijini hapo, Waziri Hasunga alimweleza Prof. Shaukat kuwa serikali ya Tanzania inaendelea na mchakato wa kubaini wafanyabiashara wanaouza mbegu feki kwa wakulima, kwa kuwa wanasababisha hasara kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi duniani ambazo wananchi wake wamekuwa wakiuziwa mbegu feki jambo ambalo serikali imelichukulia maanani na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria.

Waziri Hasunga pia alisema pamoja na Wizara ya Kilimo kuendelea na mchakato wa kuboresha kilimo kwa kutumia teknolojia mpya, bado inakabiliwa na uuzwaji wa viuatilifu feki, jambo ambalo limefifiisha juhudi za wakulima kwa muda mrefu.

"Wananchi wetu wanajitahidi kulima kwa kiasi kikubwa, lakini kumekuwapo na changamoto kubwa ya viuatilifu na mbegu feki. Jambo hili hatuwezi kuliacha na hivi karibuni nimetangaza kiama na wafanyabiashara wanaosambaza kuwa tutakapowabaini tutawachukulia hatua kali sana," alisema.

Pia alisema wakulima wengi nchini wamekuwa wakitumia mazao yao kama mbegu badala ya kutumia mbegu mpya jambo hili linapunguza ufanisi katika uzalishaji wa mazao.

Naye Prof. Shaukat Abdulrazak alisema kukutana na Waziri Hasunga kumeimarisha maradufu ushirikiano ambao umeanzishwa kwa muda mrefu na shirika hilo.

Alisema mradi wa nguvu za atomiki duniani katika Kanda ya Afrika unahusisha nchi 45 na unajikita katika uhusiano wa ushirikiano katika mazao mbalimbali yanayozalishwa.

Alisema visiwani Zanzibar, shirika hilo limesaidia kutatua changamoto kwa kuteketeza magonjwa yote yanayoambukizwa na mbung'o.

## Naibu Waziri akerwa utendaji mbovu ardhi

**Na Munir Shemweta,** MULEBA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameshangazwa na maafisa ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba mkoa wa Kagera, kushindwa kuelewa idadi ya viwanja vilivyopimwa.

Kutokana na hali hiyo, amemwagiza Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Shaban Manyama, kufanya mabadiliko katika idara hiyo ili kupata watu sahihi watakaoisaidia idara. Mabula alikutana na kadhia hiyo juzi akiwa katika siku yake ya kwanza ya ziara yake ya kutembelea wilaya za mkoa wa Kagera kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi.

Alisema haiwezekani watendaji wa ardhi kuwa katika idara washindwe kujua ni viwanja vingapi vimemilikishwa kwa wananchi wakati agizo lilishatolewa tangu mwaka 2017 kuwa viwanja vyote viingizwe kwenye mfumo ili kuwa na takwimu sahihi.

"Hapa hakuna idara ya ardhi maana watendaji wake hawajitambui, lazima pafanyike mabadiliko na kupata watu watakaoweza kusimamia idara hii maana sekta inadidimia kwa kukosa mtu wa kuisimamia," alisema.

Aidha, Mabula aliagiza Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri hiyo kuwekwa chini ya uangalizi maalumu wa miezi sita na kubainisha kuwa serikali haiwezi kuwa na sekta isiyofanya kazi zake kwa ufanisi.

Naibu Waziri pia alishtushwa na wilaya ya Muleba kuwekewa lengo la kukusanya Sh. milioni 300 lakini imekusanya Sh. 72,870,943 pekee huku ikidai Sh. bilioni 3.3, jambo alilolieleza kuwa halikubaliki kwa kuwa serikali inakosa mapato mengi.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Shaban Manyama, alimweleza Naibu Waziri kuwa halmashauri yake imekusanya Sh. milioni 72.87 kupitia kodi ya ardhi ambazo ni sawa na asilimia 24.3 na kuongeza kuwa katika kipindi cha Februari Mosi hadi Jumatatu wiki hii, wamekusanya jumla ya Sh. 1,802,750 kutokana na kodi ya ardhi.

Naye Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Ziwa, Makwasa Biswalo, alisema Muleba inahitaji kusaidiwa kutokana na watendaji wake kutokuwa makini katika utendaji kazi.

Bioswalo alitolea mfano wa tofauti ya takwimu za umilikishwaji ardhi katika halmashauri hiyo zinazoelezwa na watendaji wa sekta hiyo kuwa ni ishara kuwa idara hiyo inahitaji msaada na kuahidi kupeleka mtu kutoka ofisi ya ardhi Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kuweka mambo sawa.

HABARI KITAIFA

# Upelelezi wadaiwa kughushi saini ya waziri wakaribia

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imeambiwa kwamba upelelezi wa kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili wafanyakazi watano wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) unakaribia kufikia mwisho.

Kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali, Jenipher Massue, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi unakaribia kufikia mwisho na maendeleo ya kesi hiyo ni mazuri.

"Mheshimiwa Hakimu kesi hii upelelezi wake unakaribia kufika mwisho na maendeleo ni mazuri. Tunaomba tarehe nyingine ya kutajwa ili kuja kuangalia kama tutakuwa tumekamilisha kipengele kilichobakia," alidai Wakili Massue.

Wakili wa Utetezi, Bernard Mbakileki, aliwaomba mawakili wa serikali siku ya tarehe nyingine ya kesi hiyo waje na taarifa nzuri zaidi ili kila upande ujue hatima yake katika kesi hiyo.

Hakimu Mtega alisema kesi hiyo itatajwa Machi 27, mwaka huu, na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Wafanyakazi hao wanakabiliwa na mashtaka sita ya uhujumu uchumi likiwamo la kughushi saini ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, katika vyeti vya tathmini ya uharibifu wa mazingira na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, hivyo na kusababisha hasara ya Sh. milioni 160.

Washtakiwa hao ni Ofisa wa Mazingira NEMC, Deusdedit Katwale (38) na Mtaalamu wa IT, Luciana Lawi (33) wote wakazi wa Ubungo Msewe, Katibu Muhtasi wa NEMC, Edna Lutanjuka (51) Mkazi wa Mbezi Beach St Gasper, Msaidizi wa Ofisi Mwaruka Mwaruka (42) na Ofisa Mazingira wa NEMC, Lilian Laizer (27), wote wakazi wa Ukonga Mombasa na Ofisa Mazingira wa NEMC, Magori Wambura (38) mkazi wa Bombambili.

Kwa pamoja washtakiwa hao wanadaiwa kati ya Septemba 27, 2016 na Aprili Mosi, mwaka jana, jijini Dar es Salaam, walikula njama ya kutenda kosa la kughushi.

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kuwa Oktoba 17, 2017 jijini Dar es Salaam kwa udanganyifu walighushi cheti cha tathmini ya uharibifu wa mazingira chenye namba ya usajili EC/EIA/3366 wakijaribu kuonyesha kuwa cheti hicho ni halali na kwamba kimetolewa na NEMC wakati wakijua si kweli.

Washtakiwa hao, katika shtaka la tatu wanadaiwa kuwa Oktoba, 2017 jijini Dar es Salaam kwa nia ovu, walighushi saini ya Januari Makamba katika cheti cha tathmini ya uharibifu wa mazingira chenye usajili namba EC/ EIA/3366 wakijaribu kuonyesha kuwa ni halali na kwamba kimetolewa na NEMC wakati wakijua si kweli.

Katika shtaka la nne, Lutanjuka anadaiwa kuwa Oktoba, 2017 katika ofisi za NEMC Makao Makuu, jijini Dar es Salaam, kwa kujua alitoa cheti cha kughushi cha tathmini ya uharibifu wa mazingira chenye namba ya usajili EC/EIA/3366 cha Oktoba 17, 2017 kwa Deogratius Chacha, akijaribu kuonyesha kuwa cheti hicho ni halali na kwamba kimetolewa na NEMC wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la tano, washtakiwa hao wote wanadaiwa kuwa kati ya Septemba 27 na Aprili 6, 2018 walijipatia kwa njia ya udanganyifu Sh. milioni 160 toka kwa PMM Estate (2001) Ltd kwa madai kuwa wangeweza kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira na kumpatia cheti ambacho kinatolewa na NEMC kitendo ambacho si kweli.

Na katika shtaka la sita washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Septemba 27, 2016 na Aprili 6, 2018 Dar es Salaam waliisababishia NEMC hasara ya Sh. milioni 160.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo hadi upelelezi utakapokamilika na Mkurugenzi wa Mashtaka atakapotoa kibali cha kusikiliza au kuhamishiwa Mahakama Kuu.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Onyo la wanaonyanyasa wajawazito lifanyiwe kazi

**HIVI** karibuni tumesikia mambo ambayo yanakiuka haki za binadamu hasa wanawake na mojawapo ni kuwafukuza kazi au kuwashusha vyeo wanawake wanapopata ujauzito.

Kitendo hicho kimeifanya serikali kutangaza kuwa haitakuwa na huruma kwa waajiri wa namna hiyo ambayo si kwamba wanashangaza bali wana huzunisha kwa kuwa hawajui kuwa bila vizazi hakuna taifa.

Wiki iliyopita wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema serikali haina huruma na waajiri wa namna hiyo ambao baadhi ni wa sekta binafsi.

Tunaipongeza serikali kwa kuliona hili ambalo ni unyanyasji wa kiwango cha juu ambao pamoja na kuwaumiza wanawake kimwili, unawaathiri kisaikolojia kadhalika una athari kwa watoto walio tumboni na hata watakapozaliwa kwenye mazingira hayo. Kuna taarifa nyingine kuwa wakati wafanyakazi waajiriwa hufukuza kazi au kushushwa vyeo, baadhi ya waajiri huwatumikisha kazi wanawake vibarua wajawazito bila kujali hali zao.

Wanaofanyiwa hayo mara nyingi ni wanawake wafanyakazi vibarua ambao wanatishiwa kuwa, endapo wataondoka kwenda kujifungua au kulegalega kazini kutokana na ujauzito watafukuzwa.

Vibarua hao wanatishiwa kuwa, kupata mimba ni kujitakia na ni sawa na kujifuta wenyewe, na kuonywa kuwa waamue au wachague kazi au kuzaa watoto.

Pengine wanawake wanaopata matatizo hayo ni wengi na hawana wa kuwasaidia na huenda waajiri wao wanafahamu kuwa hawawezi kuchukua hatua kutokana na uelewa mdogo na hofu ya kudai haki zao. Katika majukwaa ya kuzungumzia haki za wanawake na unyanyasi zinatolewa taarifa nyingi kuonyesha namna ambavyo ujauzito ni changamoto kwa wanawake waajiriwa.

Wanawake hasa wasio na mikataba ya ajira wanalalamaa kuwa wanaishi katika hofu muda wote na kubeba mimba kwa kificho na wakati mwingine kufanyakazi ngumu, hata kama hawaziwezi kwa sababu ya kulinda kazi.

Ni wazi kuwa kama Waziri Ummy alivyosema, kuwa na ujauzito na kupata watoto ni jukumu la Kimungu na ni kazi ya maumbile kuendeleza kizazi ili kupata raia wa mataifa mbalimbali.

Hiyo ndiyo nguvu kazi, walipa kodi, wapiga kura na kwa ujumla ndilo taifa, na hiyo ndiyo dunia. Kwa maana hiyo ni lazima watu wazaliwe kupitia wanawake na wanaume, ni jambo lisiloзuilika na kwa utaratibu wa uumbaji kinamama wanabakia kuwa wazazi na walezi wa watoto hao.

Tunaipongeza serikali kwa kusikia kilio cha wajawazito wanaonyanyaswa. Tunaomba onyo lililotolewa lifanyiwe kazi ianzishe utaratibu wa kupata taarifa za wanaonyanyasa wanawake hao ili kuwachukulia hatua. Lakini pia, tunaomba kuwe na vipeperushi na miongozo mahali pa kazi kuonya, kukemea na kupiga marufuku mazoea hayo ambayo husababisha wanawake kupata matatizo ya kisaikolojia na kimwili. Hata watoto wao kukosa lishe na maziwa ya mama kama inavyoelekezwa na wataalamu kutokana na vitisho kazini na kuwanyima mama zao muda wa kuwajali na kuwatunza.

Tunahitaji pia wanawake kuamka na kufikisha taarifa za ukandamizaji huo polisi, kwenye Idara za Ustawi wa Jamii, mamlaka za usimamizi wa usalama na afya mahali kazi na kwenye ofisi za wanasheria wa serikali kwa hatua zaidi.


Lakini yote hayo, yatafanikiwa iwapo kutakuwa na sheria za kudhibiti mienendo hiyo ambayo inaonekana sehemu mbalimbali za kazi nchini kama waziri alivyoonya.

Tungependa kuona mambo haya yakihama kutoka majukwaani na hatua zikichukuliwa mara moja ikiwa ni pamoja na serikali kuandaa muswada wa sheria na kuufikisha bungeni ili kuwe na sheria inayodhibiti aina hiyo ya unyanyasaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Unapomficha mtoto mlemavu unalenga nini, kama si ukatili?

**HUWA** mara zote nasema, mtoto mlemavu hakupenda kuzaliwa hivyo. Ulemavu unaweza ukatokana na mambo mbalimbali kwa mtoto, na hata sisi tulio katika hali nzurui ni walemavu watarajiwa.

Wapo wanaozaliwa na wakaugua, hivyo wakaishia katika ulemavu. Wengine, huenda wazazi wao hawakula vizuri katika ujauzito na wengine kutumia dawa bila ya ushauri wa kidaktari, nao wakaishia kuzaliwa walemavu.

Tujiulize, mtoto huyo kosa lake ni nini, mpaka mzazi unaamua kumficha na kuona kama umepata laana? Mtoto huyo ana haki kama wenzake na hatakiwi kufichwa ndani.

Anatakiwa kupelekwa shule kupata elimu itakayomsaidia katika maisha yake na wataalamu wa afya. Wanasema kuwa watoto walemavu wanapofikishwa hospitali, wanapatiwa mazoezi ya viungo, hata kutegemea na hali, lakini wanarudia taratibu hali zao.

Pia, watoto hao wanapopelekwa shule wanajitahidi kusoma na wamekuwa wakifanya vizuri masomoni.

Tumeona baadhi ya watoto walemavu,wana kipaji ikiwamo hata wengine kuchora kwa kutumia miguu.

Basi, kwa mtaji huo wa kifikra, wazazi wasififishe ndoto za watoto wao wenye ulemavu, bali wawapeleke shule wakajiendeleze na baadae kufikia hatua ya kuwa huru katika maisha yao na kuacha kuwa tegemezi.

Serikali daima imekuwa ikiwajali walemavu nchini na kuna baadhi ya majengo yamewekewa miundombinu, ili kuweza kuisaidia kada hiyo. Kimsingi, hivi sasa hicho ni kigezo muhimu katika ujenzi mpya nchini.

Kuna baadhi ya shule japo si nyingi, ambazo ama zina huduma maalum au shule nzima imeandaliwa kuwahudumia watoto walemavu.

Najiuliza, kama imefikia hatua hiyo, sasa inakuwaje mzazi aliyezaa mtoto mlemavu, akajihisi kukosa wajibu wa kuwapatia elimu vijana hao.

Inatakiwa wazazi wenye watoto waelemavu, kuwapeleka shule kupata elimu. Pia, wasifungiwe ndani, bali wachanganywe kucheza na wenzao, ili wachangamshe akili zao.

Pia watoto hao wasitengwe katika familia zao, kutokana na ulemavu walio nao. Inapobidi, mzazi anapompeleka mtoto katika kituo cha walemavu, hata yeye anaweza kujiingizia kipato kwa kufanya kazi.

Kama, mtoto ataendelea kufungiwa, ni vigumu mzazi kwa mzazi kujiongezea kipato, kutokana na sehemu kubwa ya muda utautumia kukaa na mtoto huyo nyumbani na kufanya ashindwe kujiongezea kipato.

Katika mtazamo huo, pia kuna nafasi ambayo ni chanya nakiri kwamba kuna watu binafsi ambao wameyaona hayo na kuanza kuchukua hata stahiki kuyakabili.

Mathalani, wapo wanaojitolea kuwa katika sura ya ndugu na marafiki wanaowajali vijana hao nao wakajihisi wanathaminiwa na umma katika heshima na utu unaostahili kindugu zaidi.

Hapo kuna watu binafsi, asasi na hata nyumba mbalimbali za ibada, ambako kumeshikilia imani zetu na matendo ya kila siku, ikizingatiwa misingi ya imani sahihi zetu kwa pamoja, inaangalia sana namna ya kuwasilisha utu kwa matendo, pia maombi sahihi kwa ndugu hawa walemavu kutoka huo ni muhimu.

Kuna jambo ambalo huwa binafsi mara nyingi nalifikiria, kwamba kama itatokea, iwe kwa baadhi ya sehemu au kujumuika kwa pamoja, kupata nguvu kubwa zaidi kuwatendea mambo fulani kwa hawa wenzetu ambao naamini hawakupenda wala kutarajia kuwa walivyo leo.

Nafahamu fika juhudi za serikali, pamoja na uwezekano wa kuwa na hoja nyingi za aina tofauti, bado zinakabiliwa na ukomo wa uwezo kiuchumi kuwahudumia wanajamii hao.

Mathalan, bado nawakumbuka sana wezetu tuliosoma pamoja huko juu, msingi wa elimu yao ukitokea katika shule maalum ya walemavu kama vile ya huko Lushoto, mkoa wa Tanga.

Vivyo hivyo, kuna Shule Maalum ya Msingi, jijini Dar es Salaam na kwingineko walikohusishwa walemavu hao..

Dunia inavyobadilika kwa kasi, nami najua nao wanahitaji kwenda na mabadiliko hayo, ili waendane na mahitaji ya maarifa na usomi uliopo, mathalan katika matumizi ya simu na kompyuta. Haya yote yanawezekana kama tutawajali ndugu hawa.

Dawa kuu ni kuwasaidia, hasa wahitaji wakuu ambao ni watoto na ufunguo wa kwanza ni mzazi na mlezi, ambao tuko nao watoto hao maisha yote na amebeba historia tangu waje duniani.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akishiriki kuswaga ng'ombe kuingia kwenye josho la Nunge lililoko wilayani Mpwampwa mkoani Dodoma jana, aliposhiriki tathmini ya kitaifa ya uogeshaji wa mifugo, ambapo hadi sasa jumla ya mifugo milioni 32 kote nchini imeogeshwa. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini, Dk. Hezron Nonga. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Serikali yatoa msimamo mkataba wa Unesco

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ametoa msimamo kuwa Tanzania iko tayari kuridhia mkataba wa mwaka 2001 kwa nchi wanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco), kuhusu uhifadhi wa urithi wa utamaduni wa majini kama masharti iliyoyatoa yatatekelezwa.

Akizungumza juzi kwenye Mkutano wa Kikanda wa Uhifadhi wa Urithi wa Utamaduni wa Majini uliofanyika katika Mji wa Malindi nchini Kenya, Kanyasu alisema mkataba huo utahusu utafutaji wa malikale zilizomo majini zikijumuisha miji iliyozama, meli, ndege, vipande vya vyungu, sarafu, mashua na boti.

Kuhusu msimamo huo, Kanyasu aliitaka Unesco iwajengee uwezo wataalamu wa uhifadhi wa urithi wa utamaduni uliomo majini ili kubaini na kuweka kumbukumbu za maeneo yote yenye malikale hizo.

Kanyasu pia alisema Tanzania inahitaji kujifunza kutoka nchi zingine zilizoridhia mkataba huo pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya nchi na ambazo hazijaridhia ili kubadilishana uzoefu na kitaaalamu.

Alitaka mkataba huo uzingatie maslahi mapana ya nchi ili usizuie uvunaji wa rasilimali zingine kwenye eneo ambalo lipo katika mkataba.

Mkutano huo uliofanyika kwa siku mbili uliwakutanisha mawaziri kutoka Tanzania, Comoro, Djibouti, Ethiopia, Madagascar, Shelisheli, Somalia Afrika Kusini, wenyeji Kenya na wajumbe kutoka Rwanda na Ertirea.

Amesema endapo mkataba huo utaridhiwa, utatekelezwa kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Unesco na Ubalozi wa Uholanzi na tayari taratibu za utekelezaji wa mpango huo zilishaanza mwaka 2006.

# Naibu Waziri aagiza ofisa ardhi atumbuliwe

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabura, ameagiza mamlaka ya ajira iliyoko chini ya wizara yake kumwondolea wadhifa wa kaimu mkuu wa idara ya ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, John Mwingira.

Mkuu huyo wa idara anadaiwa kushindwa kusimamia idara yake ikiwamo kushindwa kukusanya kodi ya ardhi na pamoja na kuingiza katika mfumo viwanja 589.

Mabula alitoa agizo hilo baada ya kupokea taarifa za utendaji wa idara za ardhi katika Manispaa ya Bukoba na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, ambazo zilionyesha kasi ndogo katika urasimishaji wa ardhi, ukusanyaji wa kodi, uingizaji katika mfumo viwanja vilivyorasimishwa na upelekaji mashauri ya wadaiwa wa kodi ya ardhi mahakamani.

Mbali na kutaka kuondolewa, pia ameagiza ofisi ya Kamishna wa Ardhi Kanda ya Ziwa, kumwandikia barua ya onyo Ofisa Ardhi Mteule wa Manispaa hiyo, Katres rwegasira, na wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Michael Paul, kutokana na upungufu huo na asipobadilika aondolewe.

"Serikali inalenga makazi ya wananchi yarasimishwe ili kuondoa migogoro ya ardhi lakini watumishi ambao watashindwa kuendana na kasi hii hatuwezi kuwavumilia. Waondolewe wawekwe wengine wenye uwezo wa kuendana na kasi iliyopo," alisema juzi akiwa ziarani wilayani hapa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa idara ya ardhi katika Ofisa Ardhi Mteule wa Manispaa ya Bukoba, Katres Rwegasira, alisema urasimishaji wa makazi ulianza mwaka 2017 na kuwa hadi sasa viwanja 4,125 vimesharasimishwa na kuwa wanategemea ifikapo mwishoni mwa mwaka huu, warasimishe viwanja 11,330 ambavyo tayari vimepimwa.

Rwegasira alisema katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, walilenga kukusanya Sh. milioni 700 za kodi ya ardhi lakini hadi sasa wamehakusanya Sh. milioni 200. Pia alisema mashauri 52 yameshafunguliwa dhidi ya wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi.

Alisema katika mwaka huo wa fedha walilenga kutoa hati miliki 1,000 lakini hadi sasa zilizokwishaandaliwa ni 313 na zingine 229 ziko katika hatua za ukamilishaji.

Kwa upande wake, Mwingira alisema kodi ya ardhi iliyokusanywa katika kipindi hicho ni Sh. milioni 29 ambayo ni asilimia 19 ya Sh. milioni 200 zilizolengwa.




**CAREER OPPORTUNITY** **(RE - ADVERTISED)**
**LOSS CONTROL OFFICER** **(1 POST)**

**Coca-Cola Kwanza Limited (CCK Ltd) is part of the only anchor bottler in Africa, (Coca-Cola Beverages Africa) in the Coca-Cola Company's global franchise system. As a multinational company dealing in fast moving consumer products, we strive to maintain world class standards in every aspect of our business. In addition, we are also committed to train and develop Tanzanian citizens, and to this end we require the services of high caliber Tanzanians to provide a leading edge to our business.**

**LOSS CONTROL OFFICER**

CCK Tanzania requires the services of a Loss Control Officer, to be based in Dar es Salaam. The incumbent will directly report to the Logistics Director.

**The successful incumbent's responsibilities will include:**

Loss Control and Risk assessment, Analyze and Investigate system data from SAP for potential risks, Implementation of site security procedures, Internal and external incidents (such as frauds, thefts etc) investigation and evidence gathering, Prepare weekly/monthly security briefing reports for management review, Ensure that all staffs, contractors and visitors adhere to the company standard operating procedures, Monitor all goods movements, Monitoring CCTV remotely and internally, Responsible for repairs and maintenance of all security equipment, Training security staff on evacuation procedure, Health and safety, Firefighting and first aid, risk and how to combat in their daily work routine, People management & development, Supervising external security companies at various company locations, Weekly meeting with security management on their performance of the contract and their staffs, Managing the company weight bridge according to Tanzania road laws.

**Key requirements:**

Certified Security Management Professional (CSMP), Leadership skills, Attentive to details, Cooperative, Understanding SHE policies and procedures, Able to work with teams and Demonstrate high integrity and honest work environment, Computer skills with strong systems and SAP understanding along with Microsoft operating tools in Microsoft office applications, Ability to perform regular work correctly and in time without follow up and guidance, Analytical, Strong Understanding of manufacturing plant operations. Minimum 5 years experience in Loss Control and Risk Management. Military / Police background is an added advantage.

**All interested applicants please submit your applications to :**
**Coca-Cola Kwanza Ltd, HR Department, P.O. BOX 7813, Dar es Salaam.**
**or email** Saugustine@ccbagroup.co.tz
**Only successfully candidates shall be contacted.**
**Closing date for all applications: 30th March, 2019**

A subsidiary of Coca-Cola Beverages Africa

215114502

# Uhaba nguzo wakwamisha mradi wa umeme

**Na Said Hamdani,** LINDI

TATIZO la upatikanaji wa nguzo za umeme kutoka shamba la uzalishaji la Mufindi, mkoani Iringa, limetajwa kuwa sababu ya kukwama kukamilisha miradi ya usambazaji umeme vijijini kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya State Grid, inayosambaza umeme unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa Mikoa ya Lindi na Morogoro, Charles Mlawa, aliyasema hayo jana kwa mwandishi wa habari hii mjini hapa.

Alisema changamoto ya upatikanaji wa nguzo, imekuwa chanzo cha kuchelewa usambazaji umeme katika maeneo ambayo kampuni yake imepewa kazi hiyo.

Mlawa alisema wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, mkoani Lindi, wananchi walioko katika vijiji alivyokuwa ametembelea, walilalamikia ukosefu wa nguzo na wengine wakilaumu kuwa kuna mashimo yaliyochimbwa lakini nguzo hazijasimikwa.

# Pigo lingine kwa Mbowe

INATOKA UK. 2

wakati wa mkutano wa siku mbili wa kusikiliza kero, malalamiko na migogoro ya ardhi wilayani mwake, Ole Sabaya alisema watu hao wamo kwenye orodha ndefu ya wamiliki ambao viwanja vyao vimeombewa kibali cha kufutwa.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, Kiwanda cha Mashine Tools kina deni la Sh. milioni 315.721 ambalo kinadaiwa kati ya mwaka 2010 na 2018. "Huko nyuma, watu walipewa viwanja 52 vikubwa, wakaambiwa waendeleze kwa sababu ni eneo la viwanda, wana miaka mingapi? Ofisa Ardhi yuko wapi? Njoo, nini kimetokea pale?" Ole Sabaya alihoji.

"Sasa sikilizeni huo muziki, unapewa shamba (eneo la kiwanja) mwaka 1984, mmesikia? Kabla mimi sijazaliwa, hajawahi kufanya lolote, akapewa na halmashauri ili waendeleze kujenga viwanda.

"Sasa Ofisa Ardhi ameshaandika barua ya kubatilisha hivyo viwanja. Niwaambie hapahapa, wako watu mnaowaheshimu na hawalipi kodi na leo nitawataja humu."

Katika mkutano huo, Ole Sabaya alipokea malalamiko 266 yanayohusu ardhi na kuahidi kuwa ndani ya siku mbili, yatakuwa yamepatiwa ufumbuzi.

Kabla ya kutaja majina ya wadaiwa hao, Ofisa Ardhi Mteule Wilaya ya Hai, Jacob Muhumba, alisema: "Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, wengi waliopewa vile viwanja, wengine walipewa tangu mwaka 1984, wengine mwaka 2001, wa mwisho kabisa ni mwaka 2004. Wengi hawajaendeleza, lakini pia hawalipi kodi ya ardhi."

**KAULI YA MBOWE**

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia hatua zilizochukuliwa dhidi yake, Mbowe ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alisema kwa ufupi: "No comment (sina cha kueleza) katika suala hilo, sijui (Mkuu wa Wilaya) amezungumzia wapi."

Kwenye orodha hiyo ya wadaiwa wa pango la ardhi ambayo imedaiwa kutumwa kwa Waziri Lukuvi, jina la Mbowe ni la 17 akidaiwa kumiliki kiwanja/shamba Na. 51.

Inadaiwa kuwa kiongozi huyo wa kisiasa ana deni la Sh. milioni 28.284 ambalo hajalilipa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2018, wakati Hilda Ngoye anadaiwa Sh. milioni 18.688.

# Magari ya diwani yanaswa na mbao

INATOKA UK. 2

za misitu.

Alisema roli aina ya Mitsubishi lenye namba za usajili T300 AVJ lililokamatwa na mbao, mmiliki wake bado hajatambulika na lilikuwa likiendeshwa na Mohamed Msangi likiwa na mbao 1,000 zenye thamani ya Sh. milioni 16.

Kutokana na kukamatwa na mbao hizo, kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Kifungu Na. 89, mwenye gari anatakiwa kulipia faini isiyozidi Sh. milioni 48 na isiyopungua Sh. milioni 16. Na mwenye mzigo anatakiwa kulipia Sh. milioni moja au kwenda jela miaka miwili au mwaka mmoja huku mzigo ukitaifishwa.

Alisema nguzo 244 magogo madogo yamekamatwa kwenye magari matatu ambayo mawili kati yake yalibeba nguzo 184, mmiliki wake akidaiwa kuwa Diwani wa Sabasabini, Emanuel Makashi.

Magari hayo ni Fuso lenye namba za usajili T444 AQX lililokuwa limebeba nguzo 110 na Fuso T 636 ATT likiwa limebeba nguzo 74 na mmiliki wake anatakiwa kulipia faini ya Sh. 3,864,000.

Ofisa huyo alilitaja gari lingine kuwa ni Fuso lenye namba za usajili T133 AHE likiwa na nguzo 60 lililokuwa likiendeshwa na Mashaka Mpole na mwenye gari anatakiwa kulipia faini ya Sh. 1,260,000.

Akizungumzia sakata hilo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, alisema mbao na nguzo hizo zimekamatwa kwa ushirikiano wa wananchi, maofisa wanyamapori, maofisa misitu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu.

# UDSM kigugumizi rushwa ya ngono

INATOKA UK. 2

uliunda kamati ya kuchunguza ukweli wa suala hilo, huku Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) nayo ikijitosa kuzichunguza.

Akizungumza na Nipashe juzi kuhusu maendeleo ya uchunguzi wa kamati iliyoundwa na chuo, Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema inaendelea na uchunguzi.

Hata hivyo, Prof. Anangisye alisema wanajiuliza kama kuna haja ya kuweka wazi au la ripoti ya uchunguzi pindi kamati itakapokamilisha kazi yake na kukabidhi kwa uongozi.

"Bado (kamati) inaendelea na uchunguzi, hawajakamilisha, ndiyo maana hadi sasa hawajakabidhi ripoti kwetu, unajua hili suala ni nyeti, linahitaji uchunguzi wa hali ya juu na hawawezi kuliharakisha, lazima wajiridhishe. Na unapounda kamati, ujue inahitaji uhuru," alisema.

Nipashe pia ilimtafuta Ofisa Ohusiano wa Takukuru, Doreen Kapwani, ambaye alisema maofisa wao bado wanaendelea kuchunguza tuhuma hizo.

"Bado tunaendelea na uchunguzi wa jalada hili, uchunguzi bado haujakamilika," Doreen alisema.

Aprili mwaka jana, wakati wa Bunge la Bajeti, Mbunge wa Ulanga, Goodluck Mlinga (CCM), aliliambia Bunge kuwa kuna changamoto ya kuwapo kwa wahadhiri wanaofelisha wanafunzi wa kike pindi wanaponyimwa rushwa ya ngono katika vyuo vikuu mbalimbali nchini. Mbunge huyo alidai anayo majina ya wahadhiri husika na alikuwa tayari kuyakabidhi kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako.

Hii si mara ya kwanza kwa UDSM kukumbwa na kashfa ya rushwa ya ngono dhidi ya baadhi ya wahadhiri wake. Mwaka 1988, wahadhiri kadhaa waliondolewa chuoni hapo kutokana na kubainika kujihusisha na vitendo hivyo.

# JPM, mjumbe wa Putin wateta Dar

INATOKA UK. 4

na uchumi ili rasilimali na fursa zilizopo katika pande zote zitumike kwa manufaa ya wananchi wa nchi hizo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema mazungumzo hayo yamekwenda vizuri na kwamba Tanzania inatarajia tume ya pamoja ya ushirikiano ya Tanzania na Russia itasaidia kukuza uchumi kupitia madini, gesi na utalii hasa wakati huu nchi hiyo imeitangaza Tanzania kuwa nchi yenye vivutio bora vya utalii duniani. Mazungumzo hayo yalihudhuriwa na Balozi Tanzania nchi Russia,

Meja Jenerali mstaafu Simon Mumwi na Balozi wa Russia nchini Tanzania, Yuri Popov.

Wakati huo huo, Rais Magufuli alikutana na kufanya mazungumzo na timu ya wataalamu wa Tanzania na Morocco wanaoshughulikia ujenzi wa uwanja wa michezo katika Jiji la Dodoma, unaotarajiwa kujengwa kwa msaada wa Mfalme wa Morocco Mtukufu Mohammed VI.

Balozi wa Morocco hapa nchini aliyeongoza ujumbe wa wataalamu kutoka Morocco, Abdelilah Benryanen, alisema pamoja na kuzungumzia uhusiano mzuri wa Tanzania na Morocco wamejadiliana kuhusu utekelezaji wa miradi iliyokubaliwa wakati wa ziara ya Mfalme wa Morocco hapa nchini mwaka 2016 ikiwamo ujenzi wa Msikiti wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) unaojengwa jijini Dar es Salaam na kuanza kwa ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu jijini Dodoma.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Mhandisi Patrick Mfugale, alisema uwanja huo utajengwa jirani na eneo la Nanenane kando ya barabara ya Dodoma - Morogoro.

Mfugale alisema uwanja huo utajengwa kwa mfano wa Mlima Kilimanjaro na utakuwa na uwezo wa kuchukua watazamaji kati ya 85,000 na 100,005.



# Vitengo ununuzi vinara rushwa

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Songwe, imebaini vitendo vya rushwa katika halmashauri zake tano, huku vitengo vya ununuzi vikitajwa kukithiri kwa matumizi mabaya ya fedha za maendeleo.

Akiwasilisha ripoti juzi mbele ya kikao kazi cha Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa awamu ya tatu 2017-2022, kilichosimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kutoka makao makuu, Kamanda wa Takukuru mkoani Songwe, Damas Sutta, alisema vitengo vya ununuzi katika mkoa ndivyo vinaongoza kwa rushwa.

Kamanda Sutta alisema vitendo vya rushwa vimekithiri zaidi na kuathiri miradi ya maendeleo na zinakwamisha kasi ya maendeleo katika serikali ya awamu ya tano, huku akiwagusa moja kwa moja watendaji na watumishi wa umma.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, David Kafulila, kutokana na vitendo hivyo ataanza kuchukua hatua kwa kuhakikisha wanaobainika na vitendo hivyo wanachukuliwa hatua za kinidhamu.

Alisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, imejipanga kuhakikisha inawaletea maendeleo wananchi, hivyo kitendo cha viongozi kuchakachua fedha za umma hakikubaliki.

"Siku za hivi karibuni nimefanya ziara katika halmashauri zote na kubaini upungufu katika miradi ya maendeleo. Hayo yote yametokana na vitengo vya ununuzi na kwa sasa nitachukua hatua dhidi yao," alisema.

Alisema mwitikio wa wananchi katika kutoa taarifa bado ni mdogo hali inayosababisha kuwapo kwa vitendo hivyo kwa kuhofia visasi, lakini akaahidi kuwa usiri kwa mtoa taarifa unazingatiwa.

Kikao hicho kimehusisha wakuu wa idara, makatibu tawala na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa kwa lengo la kusisitiza uzalendo kwenye uwajibikaji katika utumishi wa umma.



Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita, Deogratias Matiya (kushoto), akimwonesha Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, eneo la uwekezaji la Lubambagwe (Chato Beach) wakati wa ziara ya kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi mkoani Geita. Kulia ni Meneja wa Shirika la Nyumba Mkoa wa Kagera, Benit Masika. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# Walia ushuru mkubwa samaki

**Na Anthony Gervas,** BUCHOSA

WANUNUZI wa sangara katika Halmashauri ya Buchosa, Sengerema mkoani Mwanza, wameilalamikia halmashauri hiyo kuwatoza ushuru wa Sh. 200 kwa kila kilo moja.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanunuzi wa Samaki hao, Gregory Kazimbo, alisema juzi kuwa ushuru huo ni mkubwa kwa sababu kwenye mialo wanalazimika kununua kwa Sh. 3,500 kwa kilo na kuuza viwandani kwa Sh. 4,000. "Tumepeleka maombi yetu katika halmashauri hiyo ili Baraza la Madiwani litusaidie kubadilisha ushuru huo mkubwa kwa kila kilo ya samaki Sh. 200. Tunaomba iwe angalau Sh. 30," alisema Kazimbo.

Kazimbo alisema umoja huo ulianzishwa kutoka katika mialo ya Mkoamani, Nyakaliro, Nyarusenyi, Ntama, Mchangani, Mbugani, Kanyara, Chembaya, Kabiga na Kahunda. Alisema awali walikuwa wakilipa ushuru wa jumla kwa kila tripu moja ambayo ilikuwa Sh. 100,000 lakini sasa umebadilika jambo ambalo linawaumiza katika biashara hiyo na kuwakosesha faida.

Hata hivyo, alisema wanaiomba halmashauri kuendelea kuwatoza ushuru wa jumla wa Sh. 150,000 badala ya sasa ambao unawaumiza. Alisema umoja huo hauridhiki kutozwa ushuru huo kutokana na changamoto nyingi zinazowakabili ikiwamo michango ya kijamii, kulipa kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra), ushuru wa viwandani na leseni za ukusanyaji samaki na usafirishaji.

Aidha, Kazimbo alisema bado ziko gharama nyingi zinawakabili katika jamii ikiwa ni pamoja na uchangiaji wa ujenzi wa shule, zahanati, mialo, usafi wa mazingira, ulinzi wa mialo, kulipa vibarua, mafuta na vifaa vya kuendeshea vyombo hivyo, matengenezo na usafirishaji.

# RC Mwanri awaonya watumishi wazembe

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amewaonya madaktari na wauguzi watakaozembea kuhudumia wajawazito na kusababaisha kupoteza maisha wakiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Amesema watakaobainika kuhusika na vitendo hivyo, watachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo kufutiwa leseni za kufanyia kazi.

Mwanri alitoa onyo hilo juzi alipokuwa akizindua Jukwaa la Elimu ya Afya kwa Watu wazima (Naweza) katika ukumbi wa Mtemi Isike, Mwanakiyungi mjini hapa.

Alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa kuboresha huduma za afya ya uzazi jambo ambalo limesababisha kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi, lakini baadhi ya watoa huduma wamekuwa wakifanya kazi hiyo kwa mazoea na kusababisha vifo vya mama na mtoto.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza waganga wakuu na wasimamizi wa vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuhakikisha wanaorodhesha majina ya madaktari na wauguzi watakaokuwa zamu kila siku na kufuatilia utendaji kazi wao ili kubaini wazembe.

Aliwataka kutunza vizuri kumbukumbu za mahudhurio ya madaktari, wauguzi ikiwamo wajawazito wote waliofika katika vituo vya afya kupata huduma ili litakapotokea tatizo iwe rahisi kubaini mhusika na kuchukuliwa hatua kali ikiwamo kuondolewa kazini.

Mwanri aliitaka jamii ya wana Tabora kuwa na sauti moja na kuunga mkono jukwaa hilo kwa kusema tunaweza na watakaokwamisha jitihada hizo wasifumbiwe macho. "Kuanzia sasa tutapita katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya kukagua mahudhurio na taarifa za utoaji huduma kwa wajawazito na watoto katika vituo ili kudhibiti tabia za uzembe, vinginevyo wahusika tutawaondoa," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imeendelea kuboresha huduma za afya ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na maradhi mengineyo, hivyo aliwataka watumishi hao kuacha kufanyakazi kwa mazoea.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Honoratha Rutatinisibwa, aliwataka wadau wa afya kuendelea kushirikiana na serikali na watoa huduma ili kuboresha huduma za afya ya uzazi kwa mama na mtoto katika wilaya zote za Tabora.

Alisisitiza umuhimu wa wataalamu na watoa huduma za afya kuendelea kutoa elimu ya afya na kinga kwa jamii, ili kupambana na maambukizi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo virusi vya Ukimwi (VVU).




Msukuma mkokoteni ambaye jina lake halikupatikana akiwa katikati ya Barabara ya Nyerere jijini Dodoma jana, huku waendesha magari wakijaribu kumkwepa jambo ambalo linahatarisha usalama wake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vyura wa Kihansi wapata kinga

**Na George Tarimo,** KILOLO

WATAALAMU wamegundua mbinu mpya ya kufanya vyura wa Kihansi wanaorejeshwa kwenye mazingira yao ya asili kutokea maabara kuishi bila madhara yoyote. Hatua hiyo inatokana na majaribio mbalimbali ya kisayansi yanayofanywa na wataalamu wa ikolojia na baiolojia kwa lengo la kurejesha maisha ya kawaida ya vyura hao na kuondoa hatari ya kutoweka kwa vyura hao.

Mtafiti wa vyura wa Kihansi, Dk. Charles Msuya, alisema juzi kuwa baada ya kuona vyura wengi wanaorejeshwa kwenye eneo lao la asili wanakufa au kuliwa na baadhi ya wadudu, wameanza kuwarejesha vyura wadogo na majike wenye mimba ili watoto wanaozaliwa kwenye eneo husika wazoee mazingira kwa haraka.

Alisema mkakati ambao wanaweza kusema unaonyesha mafanikio mazuri zaidi ni wa majaribio ya sasa ambayo wanatumia vyura wakubwa walitoka maabara na wenye mimba kuhifadhiwa kwenye makenji ili wazae watoto na wakishafanya hivyo, wanapata vyura ambao wamezaliwa katika mazingira halisi, hivyo kuwa rahisi kuzoea mazingira yao mapya.

"Ukizungumzia Kihansi Gorgi si chura tu kuna mazingira ambayo yana misitu yenye kuhifadhi wanyama wengi, chakula cha wanyama wakiwamo mbega, wanyama wa kila aina na mmojawapo akiwa chura, kila mnyama ambaye unaweza ukamwona katika mazingira hakuwapo kwa bahati mbaya, ana makusudi yake na ana mchango mkubwa katika mazingira lakini huwezi kujua faida ya yule mnyama kama hujaifanyia kazi," alisema.

Vyura wa Kihansi waliogundulika mwaka 1996 walianza kutoweka baada ya mradi wa kuzalisha umeme kwenye bwawa la Kihansi kuanza kufanya kazi kutokana na kupungua kwa maji ya Mto Kihansi. Maporomoko yaliyokuwa yakitengeneza mvuke wa maji ambao ndiyo maisha ya vyura hao yalikosa maji na kutokana na hali hiyo, Shirika la Umeme (Tanesco) liliachia kiasi cha maji mtoni kwa ajili ya maisha ya vyura hao.

David Mukyala, mtaalamu wa maji kutoka Bodi ya Maji Bonde la Rufiji, alisema 'catchment' hiyo ni muhimu na ina watumiaji makubwa kwa mazingira na maji kwa ajili ya uchumi kwa maana ya Tanesco kuzalisha umeme.

"Lakini sisi tumehakikisha kwamba maji kwa ajili ya ikolojia ya Gorge kule kwenye vyura ambayo si tu vyura ni ikolojia nzima kuna viumbe wengi, yanakuwapo na ndiyo maana ukichunguza kwa makini kuna maji yanaruhusiwa kutoka hapa ambayo kimsingi ni sharti la hitaji la kibali," alisema. Katika maporomoko hayo kabla ya mradi wa kufua umeme kuanza kufanya kazi, eneo hilo lilikuwa makazi asilia ya vyura wa Kihansi, lakini sasa wananchi wanaona juhudi za serikali katika kuhakikisha vyura hao wanaendelea kusihi.

Pia kuna mitambo maalumu imefungwa ili maisha ya vyura yaendelee kuwapo siku zote kwa kuwa kivutio cha taifa.

# Waandishi wakumbushwa kuzingatia sheria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAANDISHI wa habari mkoani Shinyanga, wametakiwa kuzingatia Sheria ya Huduma ya Habari wanapoandika habari zao ili kuepuka kuingia kwenye mkono wa serikali na kuchukuliwa hatua kisheria, ikiwamo kutozwa faini au kufungwa jela.

Wakili wa Kujitegemea mkoani Shinyanga, Maria Mwaselela, alitoa rai hiyo juzi, alipokuwa akitoa elimu kwa waandishi wa habari mjini hapa na namna ya kuifahamu sheria hiyo iliyotungwa mwaka 2016 ili kuitekeleza kwa vitendo.

Alisema sheria hiyo ilitungwa na serikali ili kusimamia maadili ya waandishi wa habari pamoja na kulinda maslahi ya taifa, hivyo wanahabari wanapaswa kuifahamu kwa undani ili kuepuka kuingia kwenye mkono wa serikali na kuchukuliwa hatua kali za kisheria. "Mwandishi wa habari ambaye atakiuka sheria hii ya huduma ya habari ya mwaka 2016, anaweza kufungwa jela si chini ya miaka mitano au kutozwa faini kuanzia Sh. milioni tano au vyote kwa pamoja," alisema Mwaselela kutoka kampuni ya Uwakili ya Mwaselela.

"Endapo waandishi wa habari mtaitekeleza sheria hii kwa vitendo, kamwe hamtaingia kwenye mkono wa serikali wala vyombo vyenu kuviingiza kwenye matatizo. Kwa kuitii sheria hii mtafanya kazi zenu kwa uhuru na hakuna atakayewabughudhi," aliongeza.

Baadhi ya waandishi wa habari ambao walihudhuria semina hiyo, akiwamo Moshi Ndugulile, walipongeza utolewaji wa elimu hiyo ambayo itawasaidia kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili na kutoingia kwenye mgogoro na serikali.

# Watakiwa kukutana kutatua kero za walimu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAKURUGENZI wa halmashauri za wilaya, manispaa na jiji mkoani Mwanza, wametakiwa kujiwekea utaratibu wa kukutana na wakuu wa shule za msingi na sekondari mara mbili kwa wiki ili kubaini changamoto wanazokumbana nazo na kuzitafutia ufumbuzi.

Imeelezwa kuwa hatua hiyo itasaidia kutatua kero zao mapema na kuboresha kiwango cha taaluma katika shule zao.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Michael Ligola, wakati wa hafla ya kuwapongeza walimu wa shule za msingi na sekondari wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa matokeo mazuri ya mitihani ya kitaifa ya darasa la saba, kidato cha pili na kidato cha nne kwa mwaka 2018.

"Suala la wakurugenzi kukutana na wakuu wa shule linatakiwa kutiliwa mkazo mkubwa ili kuhakikisha mkoa wa Mwanza na wilaya zake unakuwa na elimu bora kwa wanafunzi ambao watakuwa wakifanya vizuri katika mitihani yao.

Jambo hilo litawasaidia sana watoto kupenda masomo na hii yote itatokana na shule hizo kutokuwa na changamoto ambazo ziko juu ya wakurugenzi ambao ndio wanaweza kuzitatua," alisema Ligola.

Aidha, Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Seif, alisema licha ya walimu hao kufanya vizuri, bado kuna changamoto kadhaa ambazo wamejipanga kuzitatua kwa kuanzia kuwajengea uwezo walimu katika masomo ya Hisabati na Kiingereza.

Naye Mbunge wa Ilemela ambye pia ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alisema atashughulikia ombi la walimu hao la kutaka kupunguziwa malipo ya viwanja 1,600 ambavyo wametengewa katika eneo la Kabusungu ili wawe wanalipa Sh. 150,000 kila mwezi badala ya Sh. 300,000.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Dk. Saverine Lalika, aliwataka walimu hao kuijali na kuithamini taaluma mama ya ualimu na kuzishauri halmashauri zingine mkoani Mwanza kujenga utamaduni wa kuwapongeza walimu wanapofanya vizuri kwa kuwapa motisha, jambo ambalo alisema litasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa shule za msingi na sekondari.

# DC awapiga mkwara 'wanaodunga' watumishi mishale

Na Mwandishi Wetu,
MBULU

MKUU wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, amekemea tabia ya wananchi wa Bonde la Yaeda Chini kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga mishale watumishi wa serikali wanaowazuia kuchungia mifugo kwenye taasisi za umma.

Watu saba wanashikiliwa na polisi kwa mahojiano kutokana na kutenda makosa ya kuwapiga mishale watumishi wa serikali waliowazuia kuchungia mifugo maeneo ya shule.

Akizungumza na wakazi wa vijiji vya Endagulda na Domanga juzi, katika mkutano wa kutatua mgogoro wa walimu na wananchi, alisema tabia ya kuwafanyia ukatili watumishi wa serikali siyo nzuri.

Alisema walimu wa Shule ya Msingi Domanga walikimbia kituo cha kazi baada ya kutishiwa na wananchi kuwa watapigwa mishale ya sumu baada ya kuwakataza kuchungia mifugo shuleni hapo.

"Sitamuonea huruma mwananchi yeyote atakayemnyanyasa mtumishi wa umma, vyombo vya serikali vipo macho saa 24, tutawachukulia hatua na baadaye kuwalaza mahabusu," alisema.

Alisema hivi karibuni baadhi ya wananchi wa kijiji cha Endagulda walimpiga ofisa mtendaji wa kijiji hicho mshale wa sumu mgongoni kwa sababu ambazo hazijajulikana.

"Hata hivyo, nawapongeza waliompa huduma ya kwanza mtendaji huyo kwa kumnywesha mafuta ya kondoo na mkojo wa punda kisha kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Haydom kwa matibabu zaidi hadi akapona," alisema.

Alimtaka kila mkazi wa Bonde la Yaeda Chini kuwa mlinzi wa watumishi wa serikali kwa kuwa wanafanya kazi kwa manufaa ya jamii inayowazunguka na siyo vinginevyo hivyo wapewe ushirikiano.

"Hivi kweli mwalimu anamfundisha mtoto wako ili miaka ijayo akusaidie wewe, jamii na taifa kwa ujumla unaweza kumtishia maisha hadi anakimbia kituo chake ni jambo zuri hilo," alihoji.

Aliwataka askari polisi kuwachukulia hatua kali wale wote watakaofanya uvunjifu wa amani kwenye Bonde la Yaeda Chini hasa vijiji vya Endagulda na Domanga, Kata ya Eshkesh.

Hata hivyo, baadhi ya walimu wa eneo hilo walimshukuru mkuu huyo wa wilaya kwa kuwajali usalama wao kwa kuwa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu ikiwamo hofu.

Kwa muda wa wiki mbili walimu watatu wa shule hiyo waliondoka shuleni hapo na kuelekea mjini Mbulu kwa mkuu wa wilaya hiyo wakihofia vitisho vya wafugaji hao na kusababisha wanafunzi kukosa masomo.

Mmoja kati ya walimu hao, John Martin, alisema hawajawahi kuona vitendo vya ukatili kwa kutishiwa mishale sababu ya mifugo, hali iliyowalazimu kuondoka mara moja kwenye kituo cha kazi.

Aliiomba serikali kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kufanya vitendo hivyo vya kikatili kwa watumishi wa serikali ili iwe funzo kwa wengine.



Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Afya, Usalama na Mazingira migodini wa shirikisho la wachimbaji madini nchini (Femata), Dk. Bernad Joseph, akitoa elimu kwa wadau wa madini ya Tanzanite Mji mdogo wa Mirerani Wilayani Simanjiro juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ireland kukuza uchumi, biashara EAC

Na Mwandishi Wetu,
ARUSHA

BALOZI wa Ireland nchini, Paul Sherlock, amezipongeza nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kwa kuendeleza mchakato wa mtangamano na amesema nchi yake itaendelea kukuza biashara na ushirikiano wa maendeleo na nchi wanachama.

Alisema uzoefu wa Ireland katika Umoja wa Ulaya umeainisha kwamba kila mchakato wa mtangamano una changamoto zake zinatakiwa kutatuliwa kupitia mazungumzo kati ya nchi wanachama.

Alisema hayo wakati akizungumza makao makuu ya EAC jijini Arusha juzi na maofisa wa Idara ya Ushuru na Biashara waliongozwa na Balozi Alhaj Rashid Kibowa, ambaye ni Mkurugenzi wa Biashara wa Sekretariati ya EAC.

Akizungumza Alhaj Kibowa alimweleza Balozi Sherlock kwamba jumuiya hiyo imepata mafanikio makubwa kutatua vikwazo vinavyokwamisha biashara kati ya nchi wanachama.

Alisema nchi zote wanachama zimekubaliana kuondoa vikwazo vya kibiashara baada ya kupitishwa kwa sheria mwaka 2017 na wadau wamekuwa wakijengewa uwezo.

Alisema jumuiya hiyo imeanza kuwekeza katika maendeleo ya miundombinu katika sekta ya barabara, reli, bandari, nishati ili kukuza uchumi na biashara.

# Kesi kupinga uchaguzi kiti cha Spika EALA yanguruma

Na Mwandishi Wetu,
ARUSHA

MAHAKAMA ya divisheni ya kwanza ya Afrika Mashariki (EACJ), imeanza kusikiliza kesi ya kupinga uchaguzi wa kiti cha uspika wa Bunge la Afrika Mashariki, (EALA), iliyofunguliwa na Serikali ya Burundi.

Uchaguzi wa kiti cha spika ulifanyika Desemba 19, 2017, ambapo Martin Ngoga kutoka Rwanda alichaguliwa kuwa spika.

Wanaosikiliza kesi hiyo ni Jaji Kiongozi Monica Mugenyi, Naibu Jaji Kiongozi Dk. Faustin Ntezilyayao, Jaji Fakihi A. Jundu, Jaji Dk. Charles Nyawello na Jaji Charles Nyachae.

Katika kesi hiyo iliyosikilizwa juzi, mlalamikaji (Burundi), alidai uchaguzi ulifanyika pasipokuwapo kwa wabunge wa Burundi na Tanzania.

Alidai kwa kufanya hivyo kwa kuvunja misingi ya sheria iliyoanzisha Jumuiya ya EAC chini ya Ibara ya 6 (d), 7 na 57 (1) na kanuni ya 12 (1) ya EALA ya utaratibu wa kanuni.

Wakili wa Burundi, Nestor Kayobera, akisaidiana na Mwanasheria wa Serikali ya Burundi, Vyzigiro Diomede, aliwasilisha mbele ya mahakama hiyo kuwa uchaguzi wa spika unaongozwa na Mkataba wa EAC na Kanuni za EALA na kwamba Ibara ya 9(4), ya mkataba huo inataka jumuiya na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Alisema suala la akidi kwa mujibu wa Ibara ya 57 na kanuni ya 12 (1) ya Kanuni za EALA inataka ikidi katika bunge hilo au kamati ya bunge zima lazima iwe nusu ya wajumbe wanaochagua na kwamba akidi lazima iwe walau moja ya tatu ya wajumbe kutoka kila nchi mwanachama.

Aidha, alidai Desemba 19, 2017, Spika wa EALA alichaguliwa bila kuwapo kwa wabunge wa Burundi na Tanzania na kwa hiyo, uchaguzi huo ulifanyika kinyume cha misingi ya sheria ya utawala bora na utawala wa sheria.

Alidai ibara ya 23 ya mkataba inatoa madaraka kwa mahakama kama chombo cha haki kuhakikisha kinazingatia sheria tafsiri sahihi ya sheria.

Akifanya majumuisho, Wakili Kayobera, alisema Spika wa EALA hakuchaguliwa kwa mujibu wa Mkataba na Kanuni za Mwenendo wa Bunge hilo na hivyo akaiomba kuamuru kufanyika upya kwa uchaguzi huo wa spika.

Kwa upande wake, Wakili Dk. Anthony Kafumbe, aliyekuwa akimwakilisha mlalamikiwa Katibu Mkuu wa EAC, alidai uchaguzi wa spika ulifanyika chini ya Sehemu ya III ya Kanuni za Mwenendo wa Bunge hilo.

Alidai Sehemu ya III ya Kanuni za Mwenendo wa EALA, kanuni ya 6 (9) (c) ya uchaguzi wa spika, siyo lazima kwa kila mmoja apige kura, hivyo, wabunge wa Burundi na Tanzania walikuwa na uhuru wa kutopiga kura.

Mahakama itapanga siku ya kutoa hukumu ya shauri hilo.






Mwenyekiti wa Bodi wa Benki ya TPB Plc, Dk. Edmund Mndolwa (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi (wa pili kulia), wakikabidhi mfano wa kadi ya ATM kwa Mwenyekiti wa Wavuvi (TFTF), Alphonce Mkama (wa pili kushoto), jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya vikundi vya wavuvi ili kupata mikopo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliotafuna fedha za chama cha akiba waanza kuzitapika

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amesema watuhumiwa wa ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 72 ambazo ni mali ya Chama cha Akiba na Mikopo cha Uswaa, wamerejesha kiasi cha Sh. milioni 29.

Akizungumza jana na wakazi wa Kijiji cha Uswaa kuhusu kurejeshwa kwa fedha hizo, Sabaya alisema kiasi hicho cha fedha kitarudishwa kwa wananchi.

"Hizi fedha zitagawiwa kwa uwiano na niwape tahadhari tu wale ambao hawajarejesha pesa walizochota katika chama hiki, tutachukua hatua kali dhidi yao," alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Kutokana na baadhi ya watuhumiwa kusuasua, Sabaya ameagiza ambao hawajarejesha fedha hizo hadi sasa, kujisalimisha Polisi Bomang'ombe kabla ya Jumatatu ijayo.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Uswaa Mamba Saccos, Emanuel Tarimo, alimweleza Mkuu huyo wa Wilaya na ujumbe wake kwamba mpaka sasa, zaidi ya Sh. milioni 100 ziko katika mikono ya wanachama.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya) hivi tunavyoongea hapa, kuna zaidi ya shilingi milioni 100 ambazo ziko kwenye mikono ya wanachama.

Zaidi aliongeza: "Mimi nashauri serikali ya wilaya itoe amri hawa viongozi waliotufikisha hapa watozwe riba ya asilimia 30 kutokana na kiasi cha fedha walichochukua."

Baada ya kikao hicho, baadhi ya wanachama wa chama hicho cha akiba na mikopo akiwamo, Isack Ulomi, aliishukuru serikali ya wilaya hiyo kwa kuingilia kati mgogoro huo.

Ulomi ameeleza kuwa mara kadhaa wamekuwa wakipata hasara ya kulipa madalali kwa ajili ya kukusanya fedha hizo bila mafanikio.

# Uhaba wa maji watikisa wananchi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MJI wa Same mkoani Kilimanjaro unakabiliwa na tatizo la uhaba wa maji ambapo kwa sasa dumu moja la lita 20 linauzwa Sh. 1000 jambo ambalo lianzidisha ugumu wa maisha kwa wananchi wa kawaida.

Baadhi ya wakazi wa mji huo wamepaza sauti, wakilalamikia uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same kushindwa kufuatilia tatizo hilo la uhaba wa maji na kufanya hali ya upatikanaji wa huduma hiyo kuzidi kuwa ngumu siku hadi siku.

Mchungaji wa Usharika wa Makasa wa Dayosisi ya Pare ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mch.Elisa Mrutu amesema hali mbaya ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo imegeuka neema kwa baadhi ya wauzaji wa maji na kuacha kilio kwa familia zisizo na uwezo wa kumudu gharama za ununuzi wa dumu moja la maji kwa Sh. 1,000.

"Mimi naweza kumudu hiyo gharama ya kununua madumu matano kwa siku, lakini je hao ambao hawawezi kununua dumu moja kutokana na kipato duni wanaishije. Viongozi wa Halmashauri na hasa idara ya maji hawajatokea hadharani kuwaeleza wananchi shida ni nini, ndio maana inabidi tupaze sauti kwa ajili ya wengi,"alisema Mch. Mrutu

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Amon Allen alisema kuna haja ya kumuomba Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa kutuma maofisa wa wizara yake kwenda katika eneo hilo kuchunguza tatizo hilo ili kuepusha wananchi kutumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo vjiji vya jirani na kuacha kuendelea na shughuli za kiuchumi.

Alipotafutwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule kuzungumzia malalamiko hayo ya wananchi alisema: "Ni kweli hali ya maji hapa mjini upatikanaji wake ni asilimia 58 tu na hilo tatizo sio la leo wala jana, ni la muda mrefu. Tatizo hilo linaweza kwisha pale ambapo mradi mkubwa tunaosubiri sasa ukikamilika.

"Wiki kadhaa zilizopita, walikuwa wakinunua maji dumu moja kwa shilingi 500, lakini nadhani wajanja wachache wamepandisha kinyemela huko mitaani. Mimi nawaomba wawe wavumilivu, mradi mkubwa wa maji utakaomaliza adha hiyo uko mbioni kukamilika."

Wakati wananchi hao wakilalamikia tatizo la uhaba wa maji, Wilaya ya Same mwishoni mwa mwaka jana, Waziri Mbarawa alitangaza kuwa mradi wa kusambaza majisafi katika Wilaya za Same na Mwanga umefikia hatua nzuri baada ya awamu ya kwanza kukamilika kwa asilimia 80.

Mradi huo utakaokwenda hadi Wilaya ya Korogwe mkoa wa Tanga, unatarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wananchi 247,500 kutoka vijiji 28 vya wilaya hizo.

Hadi utakapokamilika mradi huo unakisiwa utatumia Dola za Marekani milioni 300 na unafadhiliwa na serikali ikishirikiana na taasisi za kimataifa na mashirika ya misaada ya kimataifa kutoka nchi za Falme za Kiarabu.

Mradi huo unatekelezwa kwa gharama zinazojumuisha ufadhili wa Benki ya Kiarabu inayosimamia maendeleo ya nchi za Afrika (Badea), Mfuko wa Ofd unaojumuisha nchi zinazozalisha mafuta (Opec) na Mfuko wa maendeleo wa kimataifa wa Saud na Mfuko wa misaada wa Kuwait.

## Halmashauri yajiongeza vyanzo vya mapato

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro imebuni vyanzo vipya vinane vya mapato ambavyo vitasaidia kuinua kiwango chake cha ukusanyaji wa mapato ya ndani, baada ya kutunga na kuja na sheria ndogo ikiwamo sheria ya ushuru wa kukodi ardhi kwa ajili ya kilimo.

Vyanzo hivyo, tayari vimepitishwa na Mkutano Maalum wa Baraza la Madiwani wa Wilaya hiyo tangu Machi 6 mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi iliyowekwa katika tovuti ya wilaya hiyo, sheria hizo ndogo zitatumika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Sheria zilizopitishwa ili kutunisha mapato ya ndani ya halmashauri hiyo ni Sheria ya ushuru wa kukodi ardhi kwa ajili ya kilimo, Sheria ya usafi na mazingira, Sheria ya ada na ushuru, Sheria ya kuzuia unywaji wa pombe saa za kazi na Sheria ya ushuru wa stendi (vituo vya mabasi).

Sheria nyingine zilizopendekezwa na halmashuari hiyo ni pamoja na sheria ya ushuru wa huduma, ushuru wa madini ya ujenzi, sheria ya usimamizi na uendeshaji wa masoko na magulio na sheria ya vijiji (sheria ya serikali za mitaa mamlaka ya wilaya.

Kulingana na sheria na taratibu za nchi, sheria hizo ndogo zinaweza kuanza kutumika mara baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleimani Jafo kutia saini sheria hizo na kisha kuzitangaza katika Gazeti la Serikali.

Halmashauri za Wilaya zinaruhusiwa kufanya hivyo, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Namba 7 ya Mwaka 1982.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo ya Siha, Godson Ngomuo amenukuliwa katika tovuti hiyo akisema sheria ndogo zilizopendekezwa na kuletwa mbele yao ili kupitishwa, zina lengo la kuongeza ukusanya wa mapato ya ndani ambayo yatapelekwa katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Tumezipitia sheria zote ndogo mstari kwa mstari na kuboresha pale tunapoona panafaa kufanya maboresho na marekebisho ili kuindoa halmashauri yetu katika tatizo la kuwa na vyanzo vichache vya mapato ya ndani," alisisitiza Ngomuo.

ama

ALHAMISI MACHI 14, 2019

AFYA NA MAZINGIRA




## Hivi ndivyo vilivyo vipodozi vyenye sumu mwilini mwako

Ukurasa 14



## Kampeni nzito kitaifa dhidi ya waendekeza ngono kwa watoto

Ukurasa 18



Ukurasa 20

## Njia bora za kuepuka maradhi trakoma, vikope na kichocho



# Kituo cha aina yake Mkuranga kinacholea wenye vichwa vikubwa

Ukurasa 19

## Asilimia 29 tu ndio wana bima ya afya



Mzazi akiwa na mwanawe wakifurahia kuwa na huduma ya bima ya afya. **PICHA: MTANDAO.**

**Geneva, Uswisi**

SHIRIKA la Kazi Duniani(ILO), imetoa ripoti kwamba zaidi ya nusu ya idadi ya watu walioko duniani, wanakosa huduma za afya, huku waliobahatika kupata huduma hizo kupitia bima za afya ni asilimia 29 tu.

Ripoti hiyo inayohusu ulinzi wa jamii katika nchi 100, pia imeeleza kuwa duniani ni asilimia 68 tu ya watu wa umri wa kustaafu ambao wanapokea kiinua mgongo.

Inaelezwa, katika nchi nyingi zenye uchumi duni, kiwango cha wanaonufaika na viinua mgongo hivyo kinazidi kushuka na kwamba sasa imefikia asilimia 20.

Aidha, ripoti hiyo inafafanua kuwa ni nchi chache kwa kiwango cha asilimia 60 ziliripoti kuwa na ama mfumo au mafao ya kuwahakikishia ulinzi wa kijamii watoto.

Huo ni utafiti ulioandaliwa na kamati ya wataalamu wa ILO, ikijikita katika mapendekezo ya ILO kuhusu ulinzi wa jamii, ambayo inatoa wito wa nchi kuwa na uhakika wa kipato na huduma za kiafya kwa watu wake, kuanzia katika utoto hadi utu uzima.

Pia, inahamasisha kuwapo ulinzi kwa watu wengi zaidi iwezekanavyo.

Emmanuelle St-Pierre Guilbault, ni mwanasheria wa ILO katika Idara ya Viwango vya Kimataifa vya Kazi, anasema: "ILO iko tayari kuzisaidia nchi kushughulikia vikwazo vilivyosalia ikiwemo masuala mazito ya kifedha, katika kuelekea ulinzi wa jamii wa uhakika kwa wote."

Ulinzi wa jamii linategemewa kuwa katika agenda za mkutano mkuu wa ILO mwaka 2020.

AFYA

# Hivi ndivyo vilivyo vipodozi vyenye sumu mwilini mwako

## TFDA Kagera yalia na mipakani




Baadhi ya wazalishaji na wauzaji wa vipodozi vya asili, katika banda lao, kwenye Maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa katika viwanja vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam. **PICHA: BLOGU YA MICHUZI.**

**Na Lilian Lugakingira, Bukoba.**

MATUMIZI ya vipodozi visivyo salama yamekuwa yakiwaathiri wananchi na hasa kinamama, katika njia ya kutafuta kupendeza kimaumbile.

Katika kundi hilo la vipodozi ambavyo baadhi ni tatizo, linajumuisha mafuta, losheni, krimu, poda, manukato, rangi za mdomoni au lipstiki.

Wataalamu wanaainisha kwamba, kuwapo vipodozi salama, pia upande wa pili kuna viambata vya sumu vyenye madhara makubwa katika miili ya watu.

### TFDA Kagera

Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini (TFDA), imekuwa ikipambana na uingizwaji na matumizi ya vipodozi hivyo, ingawa baadhi ya wananchi wamekuwa wagumu kuviacha, kwa sababu za kutokujua na wengine wanajua.

Daniel Pyuza, Mfamasia wa Mkoani Kagera, anaeleza wanavyotumia fursa mbalimbali, zikiwamo maadhimisho ya Wiki ya Mafamasia Duniani, kuelimisha umma athari za vipodozi kwa afya yao.

> "Tunataka watu wapate elimu kuwa sio kila kipodozi kinafaa," anasema na kufafanua kwamba, TFDA inawajibika rasmi kusajili...

Pyuza anayeiwakilisha TFDA mkoa wa Kagera katika maadhimisho hayo, anasema wanatumia nyenzo tofauti kuelimisha, ikiwamo radio, machapisho, mikusanyiko, shule na vyuo.

"Tunataka watu wapate elimu kuwa sio kila kipodozi kinafaa," anasema na kufafanua kwamba, TFDA inawajibika rasmi kusajili, pia kudhibiti matumizi ya vipodozi nchini.

Pyuza anasema, visivyotakiwa kwa matumizi ni vipodozi vyenye viambata vya sumu na vilivyopigwa marufuku au kwisha kwa muda wake.

Anasema kuwa vipodozi ambavyo muda wake umekwisha, ni hatari kwa maana ya kemikali zilizotumika zinaweza kuwa na sumu.

Pia anataja vipodozi visiyoonyesha tarehe ya kuharibika kwamba navyo havifai, kama ilivyo kwa vile ambavyo havijaandikwa kwa lugha za ama Kiswahili au Kiingereza.

Pyuza anataja vipodozi vingi vinavyopatikana mkoani Kagera, ni losheni na krimu, ambavyo vingi vinapokamatwa vina kiambata cha sumu.

"Inaharibu ngozi, maana inaharibu kiasili ambacho hutoa rangi. Kiasili hicho kinapoharibika, mwanga wa jua unakwenda kupiga moja kwa moja kwenye ngozi na kusababisha mtu kupata madhara, ikiwamo saratani ya ngozi," anasema.

Anaeleza namna ya kuvitambua viambata vya vipodozi, ni kuangalia lebo yake na sehemu na kukagua uwapo wa viambata kisichoruhusiwa.

"Mwananchi yeyote akikuta kipodozi anachotaka kununua kimeandikwa moja ya kiambata kilichotajwa kuwa hakifai, asikinunue na badala yake atoe taarifa TFDA kwa hatua zaidi," anasema Pyuza.

Anafaanua kwamba, kuna kampuni nyingi zinazokwepa kuweka viambata vya kutambulisha ambavyo havijaandikwa uhalali wake, kama vinafaa kiafya au la.

"Tumeishaliona hili kama mamlaka na kwa kushirikiana na ofisi za wilaya na mkoa, tumekuwa tukifanya ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara kwenye maduka ya vipodozi, ili kubaini vipodozi ambavyo vina viambata hatari, lakini havijaandikwa," anasema.

### Madhara yakoje?

Anataja madhara ni mtumiaji anapokuwa mjamzito na Pyuza ana ufafanuzi: "Ndiyo maana inashauriwa sana, mjamzito asitumie dawa wala kipodozi, bila ya ushauri wa mtaalamu wa afya."

Maeneo mengi yanajumuisha madhara ya kuugua saratani kama ya ngozi, maini, ubongo, mapafu, mfumo wa damu, utumbo mpana na kibofu cha mkojo.

"Madhara mengine ni uharibifu mkubwa wa ngozi, macho, ini, mapafu na figo, maana hizo kemikali ni sumu zinazoweza kusababisha kuharibu hiyo mifumo," anaongeza.

Katika orodha hiyo, yamo madhara ya ngozi kuungua, maumivu makali, ngozi kuwa nyekundu, kutokwa vipele, kupata mzio na kuwashwa mwili mzima.

"Mhusika pia anaweza kupata magonjwa ya akili, mishipa ya fahamu hasa kichwani, uharibifu wa ubongo na mtindio wa ubongo kwa watoto wachanga na walioko tumboni.

"Hii kwa mtoto inatokana na mama mjamzito kutumia vipodozi ambavyo havifai," anasema Pyuza, akitaja hatua za madhara ni ngozi kuwa nyembamba na laini na mwisho, mhusika anapopata jeraha au kufanyiwa upasuaji, kidonda kinachelewa kupona au kutopona kabisa.

Kuna sura nyingine, anatadharisha, kuna watumiaji wanaopata madhara kama chunusi kubwa wanashindwa kufuata ushauri wa kitabibu, wakatumia kipodozi kingine chenye madhara zaidi.

Anasisitiza kuwa tatizo la kudhibiti vipodozi lipo mkononi mwa mtumiaji, huku vingi ni batili na

**Inaendelea Uk. 15**

AFYA

Inatoka Uk. 14

vinaingizwa nchini kwa 'njia ya panya.'

Hali mipakani

"Ukienda mpaka wa Mtukula (wilayani Misenyi), kuna ofisi ya TFDA, magari yote yanayokuwa yanaingia kupitia mpaka huo yanakaguliwa, ikitokea kuna watu wamekamatwa wanachukuliwa hatua" anasema.

Anataja baadhi ya hatua zinazochukuliwa kuwa ni kuteketezwa kwa vipodozi, kupigwa faini, kifungo ikithibitika mahakamani, au vyote kwa pamoja.

Pyuza anasema, baadhi ya nchi jirani zinaruhusu vipodozi vinavyokatazwa nchini, jambo linalofanya baadhi kununua vipodozi katika nchi jirani na hawagunduliki.

Anasema, wamekuwa wakifanya ukaguzi wa kushtukiza katika maduka ya vipodozi na mengine, ambayo yamegundua kasoro hizo na wanaziuza kwa siri.

"Kuna maduka tumeyabaini na tumekuwa tukifanya ukaguzi wa kushtukiza kuondoa vipodozi hivyo na wahusika kupigwa faini. Lakini, tunaendelea na elimu kwa umma kupunguza tatizo," anasema.

Anatoa mfano wa ukaguzi mwaka jana uliofanyika eneo la Kemondo Bukoba Vijijini, kulikamatwa vipodozi batili vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni moja na wahusika alitozwa faini.

Pyuza anasema kuwa tovuti ya TFDA, imeorodhesha vipodozi vyote vilivyopigwa marufuku nchini na mkoani Kagera, wilaya zilizoathirika zaidi kwa vipodozi batili anavitaja kuwa ni Missenyi na Kyerwa, zilizoko jirani na mpaka wa nchi.

### TFDA inavyojipanga

"Tunawaelimisha pia juu ya njia wanazopaswa kufuata, ili kusajili biashara zao na namna majengo wanayoyatumia katika shughuli zao yanavyopaswa kuwa," anasema Nuru Mwasulana, Mkaguzi Chakula wa TFDA, Kanda ya Ziwa.

"Hapa nchini wajasiriamali wadogo ndiyo wengi, tunataka kuona wanakua kutoka walipo na kupata mafanikio makubwa zaidi hadi kufikia kuwa wajasiriamali wakubwa," anasema.

Anasema program hiyo ni ya kitaasisi na katika Kanda ya Ziwa, watahakikisha wanafikia mikoa sita zenye jumla ya halmashauri 45.

Kaimu Meneja wa TFDA Kanda ya Ziwa, Julius Panga, anasema mamlaka hiyo inaendesha ukaguzi wa kila mara katika kuuza vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, ili kubaini vinavyouzwa bila usajili wa TFDA.

"Ukaguzi huu wa mara kwa mara umekuwa ukilenga pia kubaini kama watu wote wanaojihusisha na biashara za bidhaa zinazodhibitiwa, wana vibali na maeneo ya kuuzia au kuzalishia yamesajiliwa?" anasema kwamba, wamegundua mapugufu hayo.

# Hivi ndivyo vilivyo vipodozi vyenye sumu mwilini mwako



Baadhi ya wajasiriamali wa kusindika vyakula na vipodozi, wakipata elimu ya namna ya kuboresha bidhaa zao, kutoka kwa wataalam wa TFDA, katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA.**

Panga anasema, katika kipindi kati ya Januari na Juni mwaka jana, TFDA Kanda ya Ziwa, ilikagua majengo ya kuhifadhi vipodozi 287 na kubaini mapungufu makubwa.

"Katika ukaguzi huo, vipodozi vyenye uzito wa tani 93.21 vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh.milioni 165.8 vilikamatwa katika jiji la Mwanza na mkoa wa Simiyu," anaeleza.

"Kwa mujibu wa kanuni za TFDA, mteja anayekamatwa anauza au kuhifadhi bidhaa ambazo haziruhusiwi kuuzwa kwa mujibu wa sheria, hutakiwa kutoa faini ya asilimia 25, kama tozo ya kuteketeza bidhaa husika," anasema Panga.

### RMO Kagera

Mganga Mkuu wa Mkoa Kagera, Dk. Marco Mbata, anaeleza undani wa vipodozi, kwamba ina madhara, kutokana na madini au vinasaba ilivyo navyo kuwa havifai mwilini mwa binadamu.

"Vipodozi hivi mpaka viandikwe na daktari kuendana na ugonjwa fulani ambao vinaweza kutibu. Lakini, kama mhusika amevitumia muda mrefu hata kama aliandikiwa, lazima daktari kila baada ya muda fulani awe anavikagua," anasema.

Dk. Mbata anaeleza kemikali na madhara yake kwenye ngozi, akitoa mfano wa kumgeuza rangi mtumiaji na anaifafanua ngozi ya mwanadamu kwamba imeumbwa katika madaraja ya matatu; Ngozi ya juu, kati na chini.

Anfafanua:"Ngozi ya juu iliumbwa ili ifanye kazi ya kuzuia bakteria wakitua wanashindwa kupenya.

Kwa hiyo kutumia vipodozi, hivyo vinakwangua ngozi na hali hii inaweza kusababisha saratani ya ngozi."

Anasema mtu anapovitumia vipodozi hivyo kwa muda mrefu, vinaweza kumpatua maradhi ya figo, kwani madini yanapomuingia, yanarundikana mwilini.

"Pia, mhusika anaweza kupata bakteria, kupatwa na vijipu uchungu, ngozi inaweza kuwa na michubuko kwa sababu zile nguvu zote zimeondolewa," anasema Dk. Mbata.

### Waathirika

Marry Michael, mkazi wa Mafumbo katika manispaa ya Bukoba ni miongoni mwa watu walioathiriwa na matumizi ya vipodozi visivyo salama.

Mama huyo anasema alianza kuvitumia na kuendelea vizuri lakini baadae vilimuathiri mfano asipotumia mwili wake uliwasha, alipata vipele na ngozi kubabuka.

Anasema kuwa alipoona anapatwa na madhara hayo aliamua kuachana navyo na kuwa sasa anaendelea vizuri na ngozi yake ya asili imeanza kurudi kama awali.

"Nilivitumia kwa kuwa sikuwa na elimu juu ya vipodozi hivi, lakini nilipopata madhara na kulazimika kufika hata hospitali kupata tiba na kuambiwa niache kutumia, nikaacha," anasema.

Mwananchi mwingine ni Jackline James mkazi wa Nshambya pia katika manispaa hiyo, anasema yeye kawaida hutumia mafuta ya mgando ya watoto, akiamini hayawezi kuwa na madhara mwilini mwake.

"Sifahamu kama mafuta haya yana madhara katika mwili wangu, kwa kuwa naona yametengenezwa kwa ajili ya watoto basi naamini hayana madhara" anasema.

Jackline anasema kuwa, elimu aliyonayo ni kwamba akiwa mjamzito, hapaswi kutumia vipodozi vya kujichubua ngozi, maana aliambiwa akijichubua itakuwa hatari atakaposhindwa kujifungua kwa njia ya kawaida, kwani akifanyiwa upasuaji, anaweza asipone kwa wataalamu kushindwa kumshona.

"Vipodozi vinaharibu ngozi ya juu. Niliambiwa hata ukipata ajali, wataalam wanaweza kushindwa kukushona na kujikuta unapata madhara makubwa zaidi au wakati mwingine kusababisha kifo" anasema. Hivyo, Jackline, anaona elimu na ushauri vitolewe juu ya madhara yatokanayo na vipodozi vyenye viambata vya sumu, kwa kuathiri wajawazito tu, hata wasio wajawazito.

"Kuna mtu unakutana naye ngozi imejaa mabaka, hayaeleweki mpaka unaogopa, ukifuatilia utakuta katumia vipodozi visivyo salama, elimu izidi kutolewa ili watu wafahamu ni vipodozi vipi wanapaswa kutumia, kila mmoja kulingana na ngozi yake," anasema.

Pia, Stella Charles, mkazi wa Kashai katika Manispaa ya Bukoba, anasema huangalia namna kipodozi anachotaka kununua kina nembo ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), basi maana vitu vingine hana uwezo wa kuvibaini na kama hakina hanunui.

Aidha, analalamikia lugha inayoandikwa kwenye baadhi ya vipodozi kuwa ni kikwazo, kwa kuwa baadhi zinaandikwa katika namna isiyoeleweka na baadae kuwaingiza wahusika katika madhara.

Mkazi mwingine wa Manispaa ya Bukoba, Claudia Bambanza, anasema hana uwezo wa kufahamu kuwa kipodozi husika hakiruhusiwi na kwamba anachokiona kinampendeza, kinafaa kutumika.

"Tunaathirika kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kugundua kama havifai, wanaohusika na udhibiti wawe makini, maana sisi tunaona hizo ndizo bidhaa nzuri za kutumia" anasema.

### Wanaume je?

Kinababa nao hawakuwa nyuma kama anavyozungumza Justine Kaijage, kuwa walio wengi wananunua vipodozi kwa kufuata harufu na marashi yenye mvuto.

"Lakini habari ya wananchi kujua madhara bado uelewa ni mdogo na ndiyo maana kuna wataalam wenye ufahamu wa haya masuala, wadhibiti ili visivyoruhusiwa kwa matumizi visiingizwe" anasema.

Anasema binafsi hawezi kuruhusu mke wake kutumia vipodozi hivyo, lakini akadai anaweza kujikuta anavitumia kutokana na kushindwa kupambanua.

AFYA

# Kinamama Tasaf watumia maadhimisho kusaidia wenzao Hospitali Mwananyamala

- Wafika na orodha ya vifaa vya kujifungua
- Daktari ataja changamoto yake kuu nafasi



Ofisa Ufuatiliaji na Mawasiliano wa Tasaf (katikati), Ntuli Mwaipopo, akikabidhi zawadi kwa wanawake wajawazito katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake katika Hospitali ya Rufani Mwananyamala. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**



**Na Elizabeth Zaya**

KATIKA kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani kila mwaka, Machi 8, ambayo kinamama duniani huungana kwa pamoja kusherehekea siku hiyo muhimu kwao.

Katika siku yao muhimu, wanawake hufanya shughuli mbalimbali za kijamii, kwa vitendo ikiwamo kutoa misaada mbalimbali.

Baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na kutembelea na kutoa misaada kwa makundi yenye uhitaji, kufanya usafi katika maeneo mbalimbali yanayotoa huduma za kijamii.

Katika baadhi ya mashirika na taasisi mbalimbali, huwaachia wanawake kuendesha shughuli za uzalishaji mali, kama kitendo cha kuonyesha uwezo wao, kwamba wanaweza hilo limekuwa likishuhudiwa kufanyika kila mwaka katika taasisi nyingi.

Kaulimbiu ya Siku ya Wanamke Duniani mwaka huu ni 'Badili fikra kufikia usawa wa kijinsia kwa maendeleo endelevu'.

Miongoni mwa walioitendea haki kauli mbiu hiyo na siku hiyo muhimu kwa wanawake duniani, ni wanawake wanaofanya kazi Mpango wa Kusaidia Kaya Masikini (TASAF), walitembelea wenzao walio katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, walio katika maandalizi ya kujifungua na wale ambao wameshajifungua.

> **"Ndiyo maana sisi tukaona kwamba tuje hapa hospitalini (Mwananyamala) tuungane na nyie wanawake wenzetu, ambao leo hii mko..**

Walikwenda na vifaa mbalimbali kuwasaidia wanawake hao, pia kuwatia moyo na kuwaonyesha wako pamoja, ingawa wako hospitalini na kuwapelekea huduma ya Tasaf, huko waliko.

### Neno lao

Akizungumza kwa niaba ya wanawake hao, Ofisa Ufuatiliaji na Mawasiliano wa TASAF, Ntuli Mwaipopo, anamtaja mwanamke ni mtu muhimu sana katika jamii na amebeba majukumu mengi, yanayopaswa kuungwa mkono na kila mtu.

Anamtaja mwanamke kibaiolojia na kijamii, kuwa ni mzazi, mlezi, mfanyakazi anayefanikiwa kuyatekeleza yote hayo kwa uwezo mkubwa, hivyo kuna umuhimu mkubwa kuendelea kuthamini juhudi zake hizo kwa namna yoyote.

"Ndiyo maana sisi tukaona kwamba tuje hapa hospitalini (Mwananyamala) tuungane na nyie wanawake wenzetu, ambao leo hii mko katika jukumu zito la kuleta Mtanzania mpya duniani.

"Tukaona tusije mikono mitupu, tumekuja na baadhi ya vifaa vitakavyowasaidia katika kipindi mtakachokuwa hapa, pia wengine watakaokuja watatumia.

"Tumewaletea viti vya kupumzikia wakati mnasubiri kujifungua, pamba, 'wheel chair' (baiskeli za wagonjwa) kwa ajili ya kuwabebea mnapokwenda kujifungua au baada, mashine maalum za kusaidia watoto wanaozaliwa kabla ya muda pamoja na pampasi,"anasema Ntuli na kuongeza:

"Hii tulijisikia kuwa tuje kuwatembelea nyie katika Hospitali hii ya Mwananyamala, maana tunaamini kwamba nyie kinamama ndio mmekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa miradi yetu ya TASAF.

"Mmekuwa mstari wa mbele kutunza na kupanga namna gani matumizi ya fedha nyumbani na upangiliaji wa hudumia mbalimbali katika familia yafanyike kwa ufasaha.

"Mbali na hivyo, kinamama nyie ndio wenye uwezo mkubwa wa kulea na kutunza familia na hata katika miradi yetu ya TASAF, tumelishuhudia hili.

"Wanawake wamepambana kwa kiwango kikubwa kuweka matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa kwa walengwa na ndivyo ilivyo katika sehemu nyingi, ambazo wamekuwa wakiwekwa wanawake, huwa wanafanya kazi zao kwa ufasaha, umakini na uaminifu.

"Kwa hiyo, ni lazima wapewe kipaumbele ikiwamo katika masuala ya afya kuhakikisha kwamba, wanakuwa salama, ili waendelee kuhudumia familia na jamii kwa ujumla."

Ntuli anasema, kuna umuhimu mkubwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kujenga tabia ya kusaidia watu na makundi yenye uhitaji, bila ya kujali ni msaada mkubwa au mdogo.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika moja ya ziara zake katika Hospitali ya Rufani Mwananyamala. **PICHA: MAKTABA.**

Daktari Mwananyamala

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Rufani Mwananyamala, Dk. Daniel Nkungu, anasema miongomi mwa changamoto zinazoikabili hospitali, ni ukosefu wa nafasi ya kutosha kuweka vitanda vinavyotosheleza idadi ya kinamama wazazi na watoto wao.

Anakiri kutambua umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kinamama waliojifungua na wanaotarajia kujifungua, wanakuwa katika mazingira yenye nafasi ya kutosha, lakini katika uhalisia, Mwananyamala kunakabiliwa na changamoto hiyo.

Dk.Nkunga anafafanua; "Tunawashukuru sana wanawake wa TASAF kwa kuja kututembelea leo, lakini kwa sababu mna mapenzi mema na wanawake wenzenu na mmejionea mazingira yaliyopo, hapa sisi Mwananyamala changamoto inayotukabili ambayo tunaweza kusema ndiyo kubwa siyo uchache wa vitanda, vitanda vipo vingi sana, isipokuwa nafasi ya kuviweka ndiyo haipo.

"Tuna nafasi finyu mno, yaani hatuna jengo lenye nafasi kubwa la kuweka hivyo vitanda. Tuna jengo ambalo liko kwenye ujenzi, ambalo tunaamini kwamba likimalizika, changamoto itakwisha kabisa," anasema Dk Nkungu.

"Niwaambie tu kwamba, hii Hospitali ya Mwananyamala inategemewa sana, karibu kila mtu anayeugua, anakuja hapa na hii huenda inasababishwa na hospitali hizi ndogo kushindwa kufanya kazi yake kwa bidiii na ndio maana tunajikuta tunapokea wagonjwa wengi kupita kiasi na hata nafasi kutotosha.

"Tunaamini kwamba, hata hizi zahanati za mtaani zingekuwa zimeboreshwa kutoa huduma bora, huu wingi wa watu tunaopokea hapa ungepungua. Kwa hiyo, niwatie moyo tu kwamba wanawake watakuwa katika mazingira bora zaidi ya kujifungua, jengo likikamilika."

> **"Tuna nafasi finyu mno, yaani hatuna jengo lenye nafasi kubwa la kuweka hivyo vitanda. Tuna jengo ambalo liko kwenye ujenzi...**

Watoto je?

Dk. Nkungu anasema, mbali na wajawazito, kundi jingine la wagonjwa lenye idadi kubwa na lenye uhitaji wa nafasi ya kutosha ni watoto.

"Kama mlivyoona ufinyu wa nafasi kwa kinamama wajawazito, hali hiyo pia ipo hata kwa sehemu ya watoto: anasema Dk.Nkungu na kuongeza:

"Hali hii kwa namna moja au nyingine, inaweza kusababisha athari hasa kwa magonjwa ya kuambukiza, kwa sababu wagonjwa wanapobanana, uwezekano wa kuambukizana magonjwa ni mkubwa."

Dk. Nkungu anahitimisha kwa kuwapongeza na kuwashukuru wanawake wa TASAF kwa msaada huo na kuelekeza wito kwa makundi mbalimbali, kujenga tabia ya kusaidia watu wenye uhitaji wa aina yoyote.

# Wazazi Italia wasiopeleka chanjo watoto kukiona



Huduma ya chanjo kwa watoto nchini Italia.. **PICHA : MTANDAO.**

NCHINI Italia kumetangazwa iwapo atatokea mtoto yeyote ambayeb hajakamilisha chanjo zake, ni wazazi na walezi wao watakumbwa na msukosuko wa kisheria, wa kutotimiza agizo hilo ambalo ni lazima kutekelezwa.

Ni agizo linaloendana pia na mzazi asiyekamilisha chanjo ya mwanawe, huenda atapigwa fanili ya Dola za Marekani 560 au sawa na Sh. Milioni 1.2, ikiwagusa zaidi watoto wenye umri chini ya miaka sita, kama ilivyoasisiwa na Waziri wa Afya wa zamani,

Maeneo ya chanjo yanayofanyiwa kazi yanajumuisha tete kuwanga na polio, ingawa wanafunzi wa chekechea hawataguswa na utekelezaji wa agizo hilo

Kwa mujibu wa agizo la serikali, ni kwamba watoto hao wazazi wao ndio watakabiliwa na mtihani huo wa kisheria. Siku ya mwisho ambayo wazazi hao walipewa ni Jumapili iliyopita.

"Sasa imekifika wakati kila mmoja anatakuiwea kuendana nayo (agizo)," anasema Waziri wa Afya, Giulia Grillo, anayedokeza, Naibu Wake Matteo Salvini, alikuwa akimtaka asogeze tarehe ya mwisho kutekeleza agizo hilo.

Katika msukosuko unaoelezwa ni utekelezaji wa agizo hilo, katika eneo la Bologna, mamlaka za serikali ya mitaa zimetoa barua kwa wazazi kuwasimasisha wanafunzi 300 kwa sababu ya kukosa chanjo.

Ni sheria inayotekelezwa, ikiwa ni sehemu ya maelekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO), kutaka walau nchi zijitahidi kupandisha kiwango cha kutekeleza chanjo za watoto kutoka chini ya asilimia 80 za sasa, hadi lengo la zaidi ya asilimia 95.


Hata hivyo, serikali ya Italia imetoa taarifa kwamba, kwa watoto waliozaliwa kuanzia mwaka 2015, wameshafikisha malengo ya kufanyiwa chanjo kwa asilimia 95.

Hata hivyo, kuna sura nyingine ya kisiasa, kwamba kuna vyama viwili vilikuwa vinapigana kupinga sheria na sera, huku kiongozi mmoja wa kisheria akikiri kwa kauli: "Ni sheria ambayo katika uidhinishaji wake tulipiga vikali.'

AFYA

# Kampeni nzito kitaifa dhidi ya waendekeza ngono kwa watoto

- Watafiti wanakadiria mabinti theluthi
- Iringa, Dar zanyooshewa vidole vibaya



Baadhi ya watoto wanaohitaji kulindwa. **PICHA: MAKTABA.**



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi. **PICHA: MAKTABA.**

**Na Yasmine Protace**

KUNA watu wanaotafsiri dhana ya ukatili ni vitendo vya kupigwa wanawake, mimba za utotoni na wanawake kukosa sauti katika maeneo wanayofanya biashara na sehemu za kazi kwa jumla, kwani unaongezeka kwa kiasi kikubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya TGNP - Mtandao, Liliani Liundi, anafafanua tafsiri hiyo akisema ukatili dhidi ya watoto ni sehemu ya maisha ya watoto wengi nchini, ambao kwa kiasi kikubwa wanakumbwa na ukatili wa kingono.

Ni ufafanuzi aliyoutoa hivi karibuni alipozungumza na wanahabari wakati wa kutoa tamko la kampeni iliyandaliwa na TGNP Mtandao dhidi ya ulinzi wa mtoto kingono, itakayojulikana kama "155 Namlinda Mtoto."

Liundi anaongeza kuwa, mwaka 2011 nchi ilitoa taarifa ya utafiti uliofanyika kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto na anafafanua, ripoti ilivyo:

"Utafiti huo umegundua kuwa karibia mmoja kati ya wasichana watatu; na mmoja kati ya wavulana saba; wamekutana na ukatili wa kingono kabla ya kutimiza miaka 18." Anafafanua kwamba kulingana na utafiti huo, sehemu kubwa ya watoto hawatoi taarifa ya vitendo hivyo na wanaofanyiwa ukatili ni wachache zaidi na wanafanikiwa kupata matibabu au msaada wanapotoa taarifa ya matukio hayo.

> **"Vitendo hivi havikubaliki katika jamii, kwani ni kinyume cha haki za binadamu na mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda iliyoridhiwa na serikali juu ya ulinzi wa mtoto...**

### HALI I LIVYO

Lilian anasema, ripoti iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu,(LHRC), zinaonyesha kuwa matukio ya ukatili wa kingono miongoni mwa watoto yanaongezeka nchini.

Ripoti hiyo ya LHRC ya Juni mwaka jana, wastani wa watoto 394 wamebakwa kila mwezi, katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara.

Inaelezwa kuwa, matukio ya ulawiti wa watoto yameongezeka kutoka 12 kwa kipindi cha Januari hadi Juni, mwaka 2017 hadi matukio 533 kama hicho mwaka uliofuata 2018 na mikoa inayoongoza kwa matukio hayo ni Dar es Salaam na Iringa.

"Vitendo hivi havikubaliki katika jamii, kwani ni kinyume cha haki za binadamu na mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda iliyoridhiwa na serikali juu ya ulinzi wa mtoto dhidi ya aina zote za ukatili wa kijinsia," anasema.

Lilian anataja baadhi ya mikataba hiyo, ni pamoja ya Haki za Watoto ya Mwaka 1989, Tamko la Afrika la Haki na Ustawi wa Mtoto la Mwaka 1990.

Analaumu kwamba vitendo hivyo vinarudisha nyuma maendeleo ya watoto na taifa kwa jumla na miongoni mwa athari zitokanazo na ukatili wa kingono dhidi ya watoto ni pamoja na watoto kuathirika kisaikolojia, maambukizi ya magonjwa ya zinaa na Ukimwi.

Anazitaja athari zingine ni mimba za utotoni zinazohatarisha ustawi wa nchi na kuchochea ongezeko la vitendo vya ukatili kwa jamii.

Kiongozi huyo wa TGNP Mtandao, anasema takwimu hizo zinaonyesha uwepo wa athari kubwa jambo linalochangia msukumo wa kampeni aliyoizindua kumlinda mtoto.

### KAMPENI IKOJE?

Lilian anasema, kampeni hiyo itachangia jitihada za serikali kutokomeza ukatili dhidi watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), unaolenga kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Anaitaja kuwa ni kampeni inayolenga kuendelea kutoa elimu kwa Jamii, juu ya athari za ukatili wa kingono kwa watoto na umuhimu wa kuwalinda dhidi ya aina hiyo ya ukatili, pia kutathmini na kuibua mjadala wa kijamii.kuhusu uhalisia wa ukatili wa kingono.

Lilian anasema kuwa ni kampeni itakayoendelea kuihamasisha jamii kuhakikisha ukatili wa kingono hauendelei na jamii kutoa taarifa tu mara waonapo matukio ya ukatili wa kingono, ili wahusika wachukuliwe hatua haraka.

Kwa mujibu wa Lilian, ni kampeni inayolenga kujenga nguvu za pamoja na wadau mbalimbali nchini, katika kuweka mikakati ya pamoja ya ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili wa kingono, ikiwamo kuhakikisha kila jamii inakuwa na wajibu wa kumlinda mtoto.

Pia, kuna dira ya kampeni hiyo ikiwa na mtazamo wa kuwafikia mwanamke, vijana, wasichana, viongozi wa dini, serikali, jamii, vyombo vya habari, madawati ya jinsia na asasi za kiraia,wabunge na wanasiasa.

Maeneo mengine yanayotajwanni wadau wa maendeleo, makungwi, watoa huduma za afya, watoa huduma za usafiri wa umaa kama vile bodaboda, na madereva wa daladala.

Mkuu huyo wa TGNP Mtandao, anaiasa jamii kuwa ina wajibu wa kuwalinda watoto dhidi ya matukio na vitendo vya ukatili wa kijinsia, kwa mujibu sa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na Mpangokazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili kwa Watoto na Wanawake.

Anasema malengo endelevu ya TGNP - Mtandao, ni kuitaka jamii iguswe na tatizo la ukatili wa kingono kwa mtoto, wakiwa nje na ndani ya shule, jamii iwajibike kuchukua hatua za kumlinda mtoto kila mahali anapokuwapo.

Anasema serikali kuu na ya mitaa, pia vyombo vya dola vinapaswa kusimamia kikamilifu Sheria ya Kudhibiti Uchawi wa Mwaka 1998, ambayo imeainisha vitendo vya watu wanaoendesha ushirikina na vinavyoweza kuwadhuru watoto kwamba navyo vinaongeza ukatili wa kijinsia, ikiwamo ubakaji.

.Lilian anahitimisha kwa kutoa rai kwa Polisi na vyombo vingine vya dola, kuhakikisha watoto wanabaki salama, kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika maeneo yote yanayotajwa kwa si salama kwa watoto.

AFYA

# Kituo cha aina yake Mkuranga kinacholea wenye vichwa vikubwa

## Mazoezi ya wagonjwa, shule, makazi wazazi



Mtoto mlemavu asiweza kutembea, akiwa katika kiti cha mazoezi. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

NI hivi karibuni akiwa wilayani Hai mkoa wa Kilimanjaro, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitoa neno kali dhidi ya wazazi wanaowanyima watoto walemavu hali zao za msingi.

Katika agizo hilo kali alilolitoa Waziri Mkuu Majaliwa alipokuwa ziarani kufungua shule ya sekondari maalum kwa walemavu, hasa pale alipoguswa na mwanafunzi Jopseph Mtei asiye na mikono na anaandika kwa kutumia mguu.

Badahi ya hali hizo za msingi anazosisitiza Waziri Mkuu zinazomhusu mtoto awe mlemavu au la, ni kupata mahitaji kama vile elimu, matibabu, malazi, mlo kamili na kutambuliwa kibinadamu, bila ya kunyanyaswa.

Kuna madai kwamba, wapo baadhi ya wazazi wanaendekeza imani na mila kwamba, watoto waliowazaa wanaangalia katika mtazamo wa mkosi na laana, wakiwafungia majumbani na hawapeleki shuleni.

Pia, kama ilivyo simulizi zilizoripowa kutoka kisiwani Tumbatu, Unguja, ambako kuna madai ya baadhi ya kinamama wanakimbiwa na waume zao wanaotelekeza familia na zigo unabaki kwa familia, hali isiyoleta matokeo bora katika haki ya mtoto.

Wilayani hapa kuna kazi iliyofanyika katika mkakati wa kuwasaidia watoto wenye vichwa vikubwa, kwa kuwaundia kituo maalum cha mazoezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho kiitwacho, Mwanangu Special Day Care and Rehabilitation Center, kilichopo Vikindu, Walter Miya, anasema watoto walemavu wana haki ya kupata elimu kama walivyo watoto wengine.

Miya anasema binafsi haoni sababu ya wazazi kuendelea kuwaficha watoto wao walemavu na kushindwa kuwapatia mazoezi na elimu. Anasema kituo chao kilianzishwa mwaka 2013 na walianza kutoa huduma za kiafya kwa watoto wenye ulemavu anayoutaja wa; vichwa vikubwa, midomo wazi, viungo na usoji.

Miya anasema mbali na Mkuranga, shirika lao linafanya kazi pia katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Manyara, ambako wanatoa huduma kwa watoto hao wenye matatizo ya kiafya wamepata matibabu na wanaendelea vizuri.

"Tunawasaidia watoto kuwapatia walimu na mazoezi na baada ya hapo wanaimarika kiafya," anasema Miya. Anasema Kituo cha Vikindu wilayani Mkuranga, kilianza huduma rasmi mwaka 2013, kikiwa na watoto zaidi ya 50, wakiwapatia elimu na mazoezi ya viungo, yanayowafanya wamudu kujishughulisha na vichwa vyao vikubwa, ambako kuna ada maalum wanawatoza hao wanaoishi katika mabweni maalum, wakiwa na utaratibu maalum ya kuwahudumia.

Pia, mbali na makazi ya watoto, wazazi wenye watoto walemavu wanaishi bure na Miya anaeleza kuwa, pia kuna huduma ya kuwapeleka watoto hospitali, mara mbili kwa wiki, huko nyumbani wakipata mazoezi ya kila siku na kisha wanaingia darasani.

> **"Tunawasaidia watoto kuwapatia walimu na mazoezi na baada ya hapo wanaimarika kiafya," anasema Miya.**

Kuhusu namna wanavyowapata watoto hao, Miya anasema huwafuata majumbani na hata mazingira mbalimbali, ikiwemo katika vyombo vya usafiri na kuwashawishi kuja kwao, baada ya kufanyika mawasiliano ya kina.

### CHANGAMOTO ZIKOJE?

Anasema kuwa, vifaa vya mazoezi ni changamoto kubwa kwao, pia rasilimali za kuendeshea huduma hiyo, kwani baadhi ya wazazi wanashindwa kuwaleta watoto, ili wahudumiwe, badala ya kuwaacha majumbani.

Jenifer Shimbusha, ni mkazi anayeishi katika kituo hicho akiwa na wanawe, anaeleza historia yake, kwamba alijifungua watoto akiwa na mimba ya miezi saba, huko Bukoba mkoa wa Kagera .

Anasema, kutokana na kukabiliwa na tatizo hilo wakati wa kujifungua, mumewe alimkimbia baada ya kuzaliwa watoto hao walioukuwa na uzito mdogo na walikuwa na matatizo ya viungo.

Jenife anasema, ni matatizo yaliyomfanya ahamishiwe katika hospitali maaluma ya CCRBT, jijini Dar es Salaam, akitokea ya Buza, nje kidogo ya jiji.

Anasema gharama za kwenda CCBRT, kutibiwa na kurudi, zilimshinda na hapo ndipo alipobahatika mbadala kupata nafasi katika kituo cha Vikindu, aliko sasa anaishi hapo na watoto anaosema wanaendelea vizuri.

### DC MKURANGA

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbert Sanga, alipotembelea kituo hicho kukagua maendeleo, anakiri kushuhudia mambo mazuri, huku akiwahimiza wananchi wake kuwapeleka watoto wenye matatizo katika kituo hicho, wakatibiwe.

Anasema wazazi wenye watoto walemavu, wanapaswa kukitumia kituo hicho, kwa kuwapeleka watoto kuhudumiwa na wazazi wakatafute riziki.

Kama alivyotamka Waziri Mkuu Majaliwa, naye anatilia mkazo kuwataka wazazi na walezi wasiwaache watoto wenye ulemavu majumbani, wapewe fursa ya kwenda kutafuta elimu.

"Wazazi wanakimbilia kuwa watoto wamelogwa wakati hayo mambo yanachangiwa na vitu vingi," anasema Sanga, katika kauli ya kuhimiza.



Mkurugenzi Mtendaji wa kituo cha kuhudumia watoto, Walter Miya, akionyesha kifaa cha mazoezi cha kinachomsaidia mtoto mlemavu, asiyeweza kusimamia.

AFYA

PATA MBINU...

# Njia bora za kuepuka maradhi trakoma, vikope na kichocho




Mgonjwa wa Trakoma.. **PICHA: MAKTABA.**

**Na Barnabas Maro**

TRAKOMA au vikope ni ugonjwa hatari uliosababisha upofu (ugonjwa wa kiumbe kutoona) kwa Watanzania wasiopungua milioni moja. Ni ugonjwa unaoshambulia macho na usipowahi matibabu, inaweza kusababisha upofu usiotibika.

Dalili zake ni pamoja na macho kuwasha, yanakuwa mekundu, yanatoa tongotongo kwa wingi, kutokana na kuuma au mtu anapoamka asubuhi.

Maambukizi ya Trakoma yanapoendelea baada ya miaka mingi, kope za macho hugeukia ndani na kukwaruza kioo cha jicho. Hali hiyo ndiyo inayoitwa ukope.

Wataalamu wa afya wana maoni kwamba, mtu anapogundua kuwa na mojawapo ya dalili hizo, asisite wala kufanya usiri katika kuchukua hatua ya kwenda kwenye kituo cha kutoa huduma za afya, kwa ajili ya uchunguzi na matibabu.

Trakoma au Vikope, inaweza kuepukwa kwa kuchukua hatua kadhaa: Mosi, ni kuhakikisha mazingira ya nyumba na choo kuwa safi kila wakati, hali inayofukuza nzi wanaofuata uchafu, kwani ndio waenezaji wakuu wa Trakoma au Vikope.

Mhusika anatakiwa kunawa kwa maji kila siku, ili kuhakikisha nzi hawatui usoni na machoni mwake. Uso wa mtu unapokuwa na tongotongo au uchafu wowote, huwavutia nzi, ambao ndio waenezaji wakuu wa ugonjwa huo.

Pia, mhusika anapaswa kuhakikisha kwamba si yeye peke yake unayenawa uso katika jumuia yake, bali wanafamilia na jamii yake, kama vile watoto wadogo; huku wakinawa uso kila mara kujikinga mara moja kwa mwaka.

### TIBA YA TRAKOMA/VIKOPE

Ili kupona, mtu anapaswa kumeza dawa maalum ya kama kinga tiba ya Trakoma/Vikope. Endapo kope zimeanza kukwaruza kioo cha jicho, mtu anapaswa kuwahi kituo cha huduma za afya na kusawazishwa kope husika, ili zisiharibu kioo cha jicho na kulipofua.

Huduma ya kusawazisha kope ni rahisi na huchukua muda mfupi tu

### KICHOCHO/ MINYOO TUMBO

Ili kudhibiti ugonjwa wa Kichocho na Minyoo ya Tumbo, inaelezwa umuhimu wa kujua jinsi ugonjwa huo unavyoenezwa.

Kichocho kuinaenezwa kupitia ama kuoga au kuogelea kwenye maji yaliyotuama, kwa maana ya kitu cha majimaji kinachoweza kumiminika kama vile maji na maziwa, madimbwi au mabwawa.

Mtu akijisaidia ovyo, nako minyoo ya tumbo inaenezwa kwa kula mboga, matunda yasiyooshwa vizuri na kula vyakula visivyoiva vizuri, hali kadhalika kutovaa viatu.

Nazo zina dawa zinazotibu na kukinga na baadhi ni za kumeza.

### ZINAVYOEPUKWA

Kichocho: Hiki kinaepukwa kwa ama kutooga au kuogelea kwenye maji yaliyotuama, madimbwi au mabwawa na kujisaidia ovyo.

Njia ya kujiweka mbali, mojawapo ni kuvaa viatu wakati wote, matumizi sahihi ya vyoo na kumeza dawa kama inavyoelekezwa na matabibu.

Minyoo: Inashauriwa mhusika kusafisha matunda na mboga kabla kuzijala, mtu anpaswa kula chakula kilichopikwa vizuri na kuiva. Mengine ni umuhimu kwa kuvaa viatu kwa usahihi na kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka, kabla ya kula na kila mtu atokapo chooni.

Kitabibu, kuna umuhimu wa mtu kumeza dawa inayotajwa mara moja kila mwaka, kuboreshe afya yako.

*** Makala hii ni kwa mujibu wa mamlaka za kiafya, chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.***

***Baruapepe: marobarnabas@yahoo.com***

***Simu: (+255) 07784 334 096.***

# Wakusanyika Nairobi kusaka teknolojia ya mazingira UN

MKUTANO wa Nne wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, umefunguliwa Jumatatu iliyopita, jijini Nairobi, Kenya, ukikusanya wajumbe zaidi ya 4,700 kutoka nchi na sehemu 170 duniani, kutafakari teknolojia za kibunifu kusimamia mazingira duniani.

Mtazamo wa ubuninfu wa teknolojia hiyo ni kuibua njia mbalimbali kutatua masuala ya mazingira na kuhimiza matumizi na uzalishaji endelevu duniani.

Mkutano huo ambao ni wa ngazi ya juu zaidi duniani, umewashirikisha idadi hiyo ya wajumbe, wakiwamo viongozi wa serikali, mawaziri wa mazingira, maofisa na wakurugenzi wa kampuni ya kimataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali, na wanaharakati wa mazingira.

Maudhui ya mwaka huu, ni kutafuta njia za kivumbuzi katika kukabiliana na changamoto za mazingira na kutimiza matumizi na uzalishaji endelevu.

Mwenyekiti wa mkutano huo, ambaye pia ni Waziri wa Mazingira wa Estonia, Siim Kiisler, anasema: "Mkutano huu utaweka mkazo katika namna ya kufanya matumizi na uzalishaji kwa njia endelevu, na kutafuta njia za kivumbuzi."



Wajumbe wa Mkutano wa Nne wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa, jijini Nairobi, Kenya juzi. **PICHA: RADIO CHINA INTERNATIONAL.**

Anasema katika miaka minne iliyopita, dunia imeshuhudia maafa mbalimbali, yakiwamo mafuriko makubwa na ukame, ambayo yamesababisha vifo vingi vya watu duniani.

"Endapo hatutachukua hatua mara moja, hatutaweza kubadilisha mwelekeo huu na kulinda usalama wa binadamu na mazingira ya asili, pamoja na utaratibu wa dunia," anasema Kiisler.

Maamuzi yatakayopitishwa kwenye mkutano huo unaomalizika kesho, yanatarajiwa kugusa kwa kina utekelezaji wa Mkataba wa Paris na Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030.

Pia, eneo lingine na matarajio ni kuondoa vikwazo kwa Mkutano wa Kilele wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa ya Umoja wa Mataifa wa mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, Joyce Msuya, anasema:"Kwanza tunapaswa kuchukua hatua haraka ili kupunguza utoaji wa hewa za ukaa na kuendeleza uchumi usio na uchafuzi wa mazingira.

"Pili, tutafikiria namna ya kupunguza athari mbaya zinazoletwa na uzalishaji wa vyakula kwa mazingira; Tatu, tukamilisha uondoaji wa matumizi ya ovyo na kuufanya uchumi wa mzunguko kuwa msukomo katika siku za baadaye." Naibu Mkuu wa Chuo cha Mazingira na Maendeleo Endelevu cha Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa na Chuo Kikuu cha Tongji, kilichoko China, Li Fengting, anasema:

"China siku zote inajihusisha katika ushirikiano wa Mataifa ya Kusini, ushirikiano na Afrika na Pendekezo la Ukanda Mmoja, Njia Moja."

Anaeleza uzoefu wake kuwa unaweza kuigwa na nchi zinazoendelea na zile zilizoendelea, akisema: "Tunatumai kueneza teknolojia zenye ufanisi na zisizo na uchafuzi wa mazingira katika nchi nyingine duniani."

Kwenye ufunguzi wa mkutano huo, wajumbe waliomboleza kwa kukaa kimya kuwakumbuka marehemu wa ajali ya Shirika la Ndege Ethiopia, iliyotokea siku chache zilizopita, baadhi walikuwa watumishi wa Umoja wa Mataifa.

Katika timu hiyo, walikuwapo wanasayansi wazoefu waliokuwa njiani kwenda kuhudhuria mkutano huo. * Habari hii ni kwa mujibu China Radio International. **UN**

# Naibu Spika atupa vijembe kwa wanasiasa

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

NAIBU Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, amewashauri wanasiasa mkoani Mbeya kuacha tabia ya kuingiza siasa kwenye shughuli za maendeleo kwa kuwa kwa kufanya hivyo kunakwamisha huduma za kijamii.

Dk. Tulia alitoa ushauri huo jana wilayani Chunya akiwa mgeni rasmi katika harambee ya kuchangia fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya cha Makongorosi, alisema wanasiasa wameingiza siasa kwenye shughuli za maendeleo hali inayosababisha baadhi ya miradi kukwama.

"Suala la kuchangia shughuli za maendeleo haliangalii umaarufu wa mtu wala itikadi ya kisiasa kwa kuwa dhana ya maendeleo haina chama na kwamba kuendekeza jambo hilo kunakwamisha ustawi wa jamii alisema," Dk. Tulia.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mary Mahundi, aliwasisitiza wananchi kuendelea kujitoa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya cha Makongorosi.

Alisema kukamilika kwa kituo hicho kutawaondolea wananchi adha waliokuwa wakiipata ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

Alisema jumla ya Sh. milioni 800 zinahitajika ili kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya ambacho kimeelezwa kuwa cha kisasa.

Aliongeza kuwa kutokana na msongamano wa wagonjwa, baadhi wanakwenda kutibiwa Mkwajuni Wilaya ya Songwe au Chunya na Mbeya, ambapo baadhi hupoteza maisha kutokana na umbali mrefu hivyo kituo hicho kitakuwa msaada kwa wakazi wa Makongorosi.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Stafford Mwakatage, alisema, kituo hicho kitakapokamilika kitatoa huduma kwa wagonjwa wa dharura, huduma za mama na mtoto na chumba cha mapumziko kwa wagonjwa wasiozidi wanne.

Katika harambee ya kuchangia ujenzi wa kituo cha afya cha Makongorosi zaidi ya shilingi milioni sitini zilipatikana huku jumla ya shilingi milioni mia nane zikihitajika mpaka kukamilika.

# Wagonjwa 500 kunufaika matibabu ya kisasa usikivu

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

ZAIDI ya wagonjwa 500, wanatarajia kupata huduma ya kisasa ya upimaji wa kiwango cha usikivu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya mwaka huu.

Huduma hiyo inakuja kufuatia hospitali kuanzisha huduma ya kisasa ya upimaji wa kiwango cha usikivu ijulikanayo kama (Pure Tone Audiometry).

Akizungumza na Nipashe jana daktari bingwa wa magonjwa ya masikio, koo na pua, Dk. Benedict Ngunyale, alisema wagonjwa walikuwa wanafuata huduma hiyo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam.

"Kwa kutumia mashine hii (Pure Tone Audiometer) itasaidia kujua kiwango cha kupoteza usikivu (hearing level) na kumwezesha mgonjwa kupatiwa matibabu ya tatizo la usikivu, tunaipongeza serikali kwa jambo hili na tumewasaidia wagonjwa kupunguza gharama kufuata huduma hiyo Muhimbili," alisema Dk. Ngunyale.

Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya imepokea msaada wa kifaa kinachotumika kufanya uchunguzi wa utumbo mpana (fiber-optic) kutoka kwa daktari bingwa wa upasuaji na mifupa kutoka Ujerumani Dk. Erhard Kirschbaum.

Akikabidhi kifaa hicho kwa niaba ya Dk. Kirschbaum, Dk. Lunemo Sakafu, kutoka hospitali hiyo alisema msaada huo ulitolewa kwa sababu ya uhusiano mzuri uliopo kwa pande hizo mbili.

Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alisema kwa sasa wamepiga hatua kwenye matibabu na uchunguzi na kwamba huduma nyingi ambazo wananchi walikuwa wanazifuata Muhimbili wanazo.

"Msaada huo umekuja kwa wakati mwafaka katika kuendeleza ufanisi mkubwa katika Idara ya Upasuaji na hospitali yetu ya kanda itaendeleza urafiki na ushirikiano wenye tija kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Tanzania hasa wa kanda hii," alisema Dk. Mbwanji.



Meneja Mawasiliano na Matukio wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Christina Murimi, akigawa vifaa kwa wanafunzi waliotembelea ofisi za Vodacom kujifunza juu ya utendaji kazi wa kidijitali wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wabadhirifu wawashiwa taa nyekundu

**Na Mwandishi Wetu,** KYELA

NAIBU Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Jumaa Aweso, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kusimamia fedha za miradi na kwamba kiongozi yeyote atakayebainika kufanya ubadhirifu achukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Aweso alitoa kauli hiyo juzi kwenye uzinduzi wa kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe, ambapo alisema baadhi ya miradi ya maji wilayani Kyela imekuwa ikalalamikiwa kuchukua muda mrefu kukamilika na kukwamisha wananchi kupata huduma ya maji.


Kutokana na changamoto hiyo aliagiza wataalamu na viongozi wa wilaya na mkoa kuhakikisha fedha za miradi ya maji zinazotolewa zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa wakati. "Nimesikia malalamiko ya wananchi kuhusu kusuasua kwa miradi ya maji hapa Kyela fedha zinatolewa na serikali, lakini hakuna kinachofanyika nawahakikishia wenye maslahi binafsi na fedha za miradi watazitapika," alisema Aweso.

Aweso alisema serikali inafahamu changamoto ya maji inavyokwamisha shughuli za maendeleo kwa wananchi wa Kyela na kwamba inaendelea na jitihada za kubuni na kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji.

Alisema miongoni mwa vyanzo vya maji vinavyotegemewa sasa ni ujenzi wa mabwawa katika mradi wa Mto Songwe ambao alidai baada ya kukamilika wananchi watakuwa na uhakika wa majisafi na salama.

Baadhi ya wananchi wilayani humo wamewatupia lawama wataalamu kwa madai ya kutowashirikisha kwenye shughuli za ujenzi ikiwamo usimamizi.

Mmoja wa wananchi hao, Lupakisyo Mwaipopo, alisema jukumu la kusimamia miradi ya maji ni kila mwananchi lakini changamoto iliyopo ni wataalamu kuwatowahusisha wananchi.





# Kada wa CCM atoa maagizo kwa halmashauri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Dodoma, Grace Shindika, ameitaka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuongeza jitihada katika utatuzi wa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa kwa wakazi wa eneo hilo hivi sasa.

Shindika aliyasema hayo jana, wakati aliokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisi kwake juu ya changamoto mbalimbali zinazolikabili Jiji la Dodoma wakati huu, ambapo linapokea idadi kubwa ya watu.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma bado haijafanya kazi kwa asilimia kubwa katika kutatua kero ya migogoro ya ardhi hali ambayo wakazi wa maeneo mbalimbali wamekuwa wakilazimika kufika katika ofisi za chama hicho ili waweze kusaidiwa.

Shindika aliongeza kuwa pamoja na changamoto nyingine zilizopo katika Jiji la Dodoma kama vile miundombinu ya barabara mibovu katika baadhi ya maeneo lakini suala la migogoro ya ardhi bado ni kero kubwa.

"Jiji bado halijafanya kazi kabisa ya kutatua migogoro ya ardhi kwa wananchi wa Dodoma migogoro hii imekuwa mingi sana hapa jijini kila kona ya eneo unakokwenda watu wanalalamika juu ya ardhi, hivyo basi wahusika wajitahidi katika kumaliza hii kero," alisema.

Alisema kutoka na ziara zake ambazo amekuwa akizifanya katika maeneo mbalimbali ya Jiji amekutana na malalamiko mengi kutoka kwa wanachi juu ya kuchukuliwa ardhi yao bila malipo.

"Kama Jiji litafanya kazi ya kuhakikisha kuwa hii migogoro inamalizwa basi hata uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu katika chama chetu tungeshinda kwa asilimia 100, lakini hali ilivyo hivi sasa ni kama asilimia 94 za ushindi," alisema.

Aidha, aliwata watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma wenye dhamana ya usimamizi wa ardhi kuacha ubabaishaji pale ambao wanapopata malalamiko kutoka kwa wananchi.

"Watumishi wanatakiwa kuwasaidia wanachi katika kuhakikisha wanapata haki zao na siyo kuwazungusha hali ambayo inawasababishia waje katika ofisi za chama ili waweze kusaidiwa wakati wao waliopewa dhamana na serikali wapo," alisema.



Mwenyekiti wa kikundi cha wajasiriamali cha Mema cha Msalato jijini Dodoma, Holanda Chipeta (aliyeshika kipaza sauti), akitoa maelezo kwa wageni waliotembelea kikundi chao kuhusu shughuli zinazofanywa kuzalisha bidhaa zao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Gwajima azungumzia umuhimu upatikanaji wa taarifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia afya Dk. Dorothy Gwajima, amesema upatikanaji wa taarifa kuanzia ngazi ya halmashauri, mikoa bado ni changamoto hali ambayo inasababisha kurudisha nyuma kasi ya ufuatiliaji wa utekelezaji mipango ya maendeleo.

Dk. Gwajima aliyabainisha hayo kwenye kikao kazi cha Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kilichofanyika katika ukumbi wa Hazina jijini Dodoma.

Alisema makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wote nchini wanatakiwa kuhakikisha kila idara inawasilisha taarifa sahihi na kwa wakati, ili kuweza kuimarisha tathmini ya kasi ya utekelezaji wa majukumu ya serikali.

"Taarifa ya mpango wa malipo kwa ufanisi (RBF) umechukua miezi 3 na cha kushangaza baada ya kutoa notisi ya saa 72 kuwa waganga wakuu wa mikoa na halmashauri wakabidhi majukumu ya uongozi iwapo watashindwa kuwasilisha na warudi kwenye kazi zao za kitaaluma wote kabla muda huo, kitu kinachodhihirisha kuwa kuna uzembe katika uwajibikaji," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe wanasimamia wataalamu walio chini yao kuwajibika kikamilifu na kwa wakati.

Akizungumzi juu ya utoaji wa taarifa za ujenzi wa hospitali mpya 67 za Halmashauri za Wilaya alisema kuwa waganga wakuu wa mikoa waliagizwa kuwasilisha taarifa hizo wiki mbili zilizopita, lakini mpaka sasa ni mikoa sita tu ndiyo imetoa taarifa. Aidha, mikoa mingine iliyowasilisha taarifa hizo hazijakamilika, hivyo amewaagiza waganga wakuu wa mikoa na halmashauri kuhakikisha wanawajibika kuwasaidia kikamilifu viongozi wao.

"Kuwe na mpango wa ujenzi wa vituo unaoonyesha nini kinafanyika kila wiki na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kila wiki wizarani," alisema.

Aidha, Dk. Gwajima alisema kuwa kila Katibu Tawala wa Mkoa husika na Mkurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ahakikishe vituo vya afya vyote vilivyokamilika vinawezeshwa kuanza kutoa huduma kwa kutumia rasilimali zao ndani badala ya kusubiri kila kitu toka serikali kuu.

Dk. Gwajima alisema kuwa kila halmashauri ihakikishe inatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato kwenye vituo vyote vya afya ili kuepusha mianya ya upotevu wa fedha za serikali. Alisema kuwa kumekuwa na tabia ya baadhi ya watoa huduma kutafuta visingizio vya kutotumia mifumo hiyo, hivyo wajue kuwa matumizi ya mifumo ni lazima na haikwepeki.

# Watanzania wapewa neno kufanya kazi kwa bidii

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Evangelisct Assembelise of God Tanzania (EAGT) Ipagala Dodoma, Evance Chande, amewataka Watanzania kufanya kazi kwa bidii ili kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali katika kufikia uchumi wa viwanda.

Chande, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza katika hafla ya kuwatunuku tuzo ya utendeji uliotukuka watumishi mbalimbali wa kiroho, kijamii, taasisi za kiraia na kiserikali iliyotolewa na taasisi ya Outreach Care. Alisema kuwa ili tuweze kufikia malengo ya Rais wa awamu ya tano ni muhimu Watanzania wakafanya kazi kwa jitihada na kujituma kwa ajili ya kufikia hatua hiyo ya uchumi utakaowezesha upatikanaji wa viwanda hivyo vya kati.

"Leo hapa tumeshuhudia watumishi hao wakipatiwa tuzo hii iliyotolewa na Outreach Care, wamepewa kutokana na juhudi zao walizozifanya ambazo zimelenga kuunga mkono jitihada za Rais wetu pamoja na kuwa walio wengi ni watumishi wa Mungu ambao pia kwa kazi yao haina tofauti katika jitihada hizo za kufikia uchumi wa viwanda," alisema. Naye Askofu wa Wolrd Ministres, Damas Thadey, aliwataka vijana kujituma katika utendaji wa kazi ili waweze kutunukiwa tuzo mbalimbali ambazo zitafanya kutambulika kiroho, kijamii na hata katika serikali.

Alisema kuwa changamoto iliyopo kwa vijana walio wengi wamekuwa hodari kwa kuionyoshea serikali vidole, huku wakiishi bila kufanya kazi hatua ambayo itawafanya kuendelea kulalamika na kushindwa kuchangia maendeleo ya taifa.

Awali akihubiri kwenye sherehe ya kutunuku tuzo za utendaji uliotukuka kwa watumishi hao wapatao 42, Askofu Mkuu wa Kanisa la Light House Christian Center, DSM, Dk. Rejoice Ndalima, aliwataka waliotunukiwa kutumia nafasi zao kuwafundisha waumini ili waweze kuwa na imani ya kiroho badala ya kuwafokea.



HABARI ZANZIBAR

# Wanawake wa CCM wafundwa kisiasa maandalizi ya 2020

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi Tanzania (UWT), umewataka wanawake wa Mkoa Kusini Unguja kutobweteka na hali ya kisiasa mkoani humo na badala yake waandae mbinu imara za kulinda ustawi wa CCM.

Akizungumza na wanawake wa CCM wa Mkoa huo, Mwenyekiti wa UWT, Gaudensia Kabaka, alisema licha ya mkoa huo kusifika kwa kuwa ngome ya CCM Zanzibar bado wanawake wana jukumu la kulinda heshima hiyo ili isichafuliwe na vyama vya upinzani.

Aliwasihi wanawake hao kuungana na kuhakikisha wanafanya kazi kwa pamoja katika kukiletea ushindi CCM katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020. Alisema mafanikio yaliyofikiwa katika CCM yametokana na juhudi kubwa za wanawake wa UWT wanaopigania maslahi ya taasisi hiyo usiku na mchana ili isonge mbele kimaendeleo.

Mwenyekiti huyo alikemea vitendo vya udhalilishaji wa watoto katika mkoa huo na kuiagiza taasisi za kisheria kuchukua hatua kwa watu wanaofanya uhalifu huo kwa kuwa unaharibu ndoto na malengo ya watoto ambao ndio taifa la baadaye.

Aidha, aliwakumbusha wanawake wa mkoa huo kuhakikisha wanakuwa wanachama hai wa CCM kwa kulipia ada ya uanachama ili pindi pakitokea nafasi yoyote ya kuwania uongozi wawe na vigezo sahihi vya kuingia katika ushindani wa nafasi hizo. Pia alisisitiza umuhimu wa UWT na CCM, kufanya uhakiki wa mara kwa mara wa wanachama ili kujiridhisha na kutambua takwimu sahihi za wanachama wao.

Naye Makamu Mwenyekiti wa UWT, Thuwaiba Kisasi, alimwakikishia mwenyekiti huyo kuwa mkoa huo una historia ya kudumu ya wanachama wake kuwa wanachama wazalendo wenye misimamo imara isiyoyumba.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akimwapisha Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Hamida Mussa Khamis, katika hafla iliyofanyika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Kampuni ya Zantel yapiga hodi hospitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya simu Zantel kwa kushirikiana na Hospitali ya Tasakhta Global Mjini Zanzibar, imezindua huduma ya kulipia matibabu kwa njia ya mtandao (Eazy pesa).

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mtendaji Mkuu wa Zantel, Mohammed Baucha, alieleza kuwa mfumo huo utawarahisishia wateja wenye Easy Pesa kupata huduma hata wasipokuwa na fedha taslimu.

Alisema kuwa taasisi hizo mbili zimeamua kuja na huduma hiyo ili kuwaondoshea wateja wa Zantel ulazima wa kutembea na fedha nyingi hali inayohatarisha usalama wao na wa pesa zao.

"Ili kupata huduma hiyo, ni lazima mtu anayehitaji awe amejisajili katika mtandao wa Zantel Easy Pesa, hivyo anawaomba wananchi ambao sio wateja wa mtandao wa Zantel kuharakisha kujiunga," alisema. Aidha, alisema afya ndio utajiri wa kila binadamu, hivyo ni lazima wateja wao kuwasogezea huduma ili malipo ya afya zao yaweze kutumika katika simu za kiganjani.

Baucha alieleza kuwa huduma hiyo ni ya mwanzo katika sehemu ya afya, hivyo alitumia muda huo kuwaomba wananchi ambao sio wateja wa Zantel kujiunga ili kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na mtandao huo.

"Global hospitali ni ya kwanza kuzindua huduma hii kwa hapa Zanzibar, hivyo wateja wetu wataweza kulipia huduma za matibabu kwa kutumia simu zao za mkononi," alisema.

Naye Ofisa Masoko wa Zantel, Haji Khatib, alisema makubaliano hayo ya pamoja baina ya Zantel na Global Hospitali ni ya moja kwa moja kwa kuwa lengo lao ni kuwafikia wateja wote wa Zanzibar kuhakikisha wanatumia huduma hiyo ili kupata matibabu kwa urahisi zaidi. Alisema kwa muda wa miaka 20 Zantel imekuwa karibu na wateja wao katika kutoa huduma mbalimbali ikiwamo huduma za sauti na hivi sasa kuanzisha huduma ya malipo ya afya kwa kutumia simu ya mkononi.

Kwa upande wake Meneja Mawasiliano wa Maendeleo ya Biashara katika Hospitali ya Tasakhta Global, Christina Sintah Manungi, alisema huduma hiyo mpya imeanza Machi 12, na kwa wateja watakaoitumia katika miezi mitatu ya kwanza, watapata punguzo la asilimia tano.

Alisema kuanza kwa huduma hiyo kutasaidia kwa kiasi kikubwa jamii kuweza kutumia huduma za kiafya kwa urahisi zaidi.

# Shule ya Lumumba yapigiwa debe ujenzi wa bweni

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Green Light Foundation imeiomba Serikali ya Zanzibar kujenga bweni katika Shule ya Sekondari Lumumba ili kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa sayansi.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Salim Mussa Omar, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika hafla fupi ya kumzawadia mwanfunzi bora aliyefaulu mitihani ya kidato cha nne mwaka huu na kupata ufaulu wa daraja la kwanza.

Alisema Shule ya Lumumba ndiyo shule pekee ya Serikali kwa Zanzibar inayotoa matokeo mazuri katika mitihani ya kidato cha nne hivyo ipo haja wanafunzi kujengewa bweni ili waweze kusoma kwa bidii wakati wote wanapokuwapo shuleni hapo.

Aidha, alisema elimu ndio msingi mkuu wa maendeleo nchini, hivyo taasisi yao itaendelea kushajihisha wanafunzi kusoma kwa bidii na kushirikiana na serikali katika kuunga mkono jitihada za kuinua kiwango cha elimu nchini.

Salim, alisema mwanafunzi huyo bora na wanafunzi wengine ni chanzo cha kupata wataalamu wa ndani hapo baadaye na kuliendesha taifa lao.

"Kwa kweli kumbe na sisi tunaweza kwa kuwa tumeshazoea kila mwaka kusikia mikoa mengine kutoa Tanzania Bara, lakini mara hii tumetoa mwanafunzi bora katoka Zanzibar na tunategemea mwakani pia tutapata wanafunzi 30 wa daraja la kwanza katika masomo haya ya sayansi," alisema.

Aidha, mkurugenzi huyo alisema lengo la taasisi yake kuwazawadia wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani yao hasa kwa masomo ya sayansi ni kushajihisha wanafunzi kupenda kusoma masomo ya sayansi ili kupata wataalamu wa baadaye waliobobea.

Katika hatua nyingine, mkurugenzi huyo, aliwaomba wazazi kuwa na utaratibu wa kufuatilia maendeleo ya kielimu kwa watoto wao jambo linaweza kuwajengea ari ya kufanya vizuri zaidi katika masomo yao.

Aliziomba taasisi nyingine kuungana na serikali katika kuhamasisha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo ya sayansi na kupata viongozi bora wa baadaye kupitia sekta mbalimbali.

Naye mwanafunzi Hassan Hamid Ussi aliyepata daraja la kwanza kwa masomo ya sanyasi, aliipongeza taasisi hiyo na kuwashukuru wazazi na walimu katika kumsaidia hadi kutimiza malengo yake, huku akiwashauri wanafunzi wenzake kusoma kwa bidii kwa maendeleo ya nchi.

Mwanafunzi huyo alizawadiwa tunzo maalum na kulipiwa ada yake ya masomo ya ziada, chakula katika Shule ya Sekondari ya Shamsia jijini Dar-es-Salam kwa ajili ya kuendelea na masomo yake ya elimu ya juu baada ya kupata udhamini katika shule hiyo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 11 March**

06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 12 March**

06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 13 March**

06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 14 March**

06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 15 March**

06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 16 March**

08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Grindstone road
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 17 March**

08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 11 March**

05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 12 March**

05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum: Ewura
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 13 March**

05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kesho Leo rpt
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 14 March**

05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi Maalum rpt: Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
09:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 15 March**

05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 16 March**

05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 17 March**

05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Tafrija ya chakula cha mchana kwa watu wenye ulemavu
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Hard Price 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


5 EATV eNewz

LEO JIONI SAA 12:00

ALHAMISI
11:00 DADAZ (live)
12:00 Mpya
15:00 FUNGUKA
16:00 Bongo Hits
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Bongo Hits



eNewz Kupata fununu, udaku na habari zote za mjini kuhusu wasanii na maisha yao, ulimwengu wa wasanaa, burudani na pia matukio yaliotokea siku kama hiyo kwenye historia ya sanaa.

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise
88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**

05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**

05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**

05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**

05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

# Moto wateketeza soko Nairobi

**NAIROBI,** Kenya

SOKO la Toi lililoko mjini Nairobi Kenya, limeteketea kwa moto na kusababisha mali za thamani isiyojulikana kupotea. Moto huo ulizuka majira ya saa tisa alfajiri katika soko hilo.

Soko hilo maarufu na linalofahamika kwa uuzaji wa bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuku, nguo za mtumba, lakini pia bidhaa nyingine kama mbao na vifaa vya elektroniki.

Baadhi ya wafanyabiashara wamelaumu Idara za Zimamoto kuchelewa kukabiliana na moto huo kwa wakati mzuri na kuudhibiti kabla ya kusambaa katika sehemu nyingine.

Mara kwa mara Idara ya Zimamoto nchini Kenya imekuwa ikishutumiwa kwa kushindwa kudhibiti mikasa ya moto kwa muda mwafaka licha ya kuwa na vifaa vipya.

Hata hivyo, taarifa kutoka Idara ya Zimamoto ilieleza kuwa magari ya zima moto yameshindwa kuingia ndani zaidi katika soko hilo kutokana na makazi yasiyo rasmi, vijiji kutokuwa na mpangilio mzuri, nyumba kusongamana sana na hakuna njia za katikati.

Wafanyabiashara katika soko hilo wameelezea masikitiko yao, huku wakieleza kuwa wamepoteza mamilioni ya fedha na kusema walitegemea biashara katika soko hilo kujikwamua kimaisha. **RFI**

# Wanamgambo 3,000 wa IS wajisalimisha

**DAMESKI,** Syria

WAPIGANAJI 3,000 wa kundi la Dola la Kiislamu (IS) wamejisalimisha kutoka kwenye ngome yao ya mwisho ya Baghouz Mashariki mwa Syria kwa vikosi vya Kikurdi, baada ya kuanza tena mashambulizi ya anga na makombora.

Wanamgambo wa Kikurdi wa Syrian Democratic Forces wanaoungwa mkono na Marekani, kwa wiki kadhaa wamekuwa wakijaribu kuwasambaratisha wapiganaji wa IS, lakini uwapo wa idadi kubwa ya wanaume pamoja na wanawake na watoto ulisababisha mashambulizi hayo kufanyika taratibu.

Tangu mwishoni mwa wiki mashambulizi ya anga yameendelea mjini Baghouz kwa siku tatu mfululizo na kuwaua wapiganaji kadhaa wa IS, hali ambayo iliwashinikiza wapiganaji wengine wa IS kujisalimisha pamoja na familia zao. Msemaji wa SDF, Mustafa Bali, alisema idadi ya wapiganaji wa IS waliojisalimisha tangu Jumatatu jioni imefikia 3,000.

Jana, SDF ilisimamisha mashambulizi hayo kwa muda katika kijiji kinachodhibitiwa na IS cha Baghouz, Mashariki mwa Syria ili kuruhusu raia kuondoka kwenye kijiji hicho na kujisalimisha. **DW**

# Marekani yasema safari za Boeing hazitasimamishwa

**WASHINGTON,** Marekani

MAMLAKA ya kuratibu safari za Ndege za Marekani (FAA), imesema haitasimamisha safari za ndege aina ya Boeing 737 Max, baada ya kutokea kwa ajali ya Ndege ya Ethiopian Airlines, ambayo iliua watu 157.

Kaimu Ofisa Mkuu wa mamlaka hiyo, Dan Elwell, alisema kwamba uchunguzi uliofanywa hadi kufikia jana, haujabaini hitilafu yoyote na mfumo wa ndege hizo, hivyo haoni haja ya kusitisha safari zake.

Kudondoka kwa ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia kumesababisha nchi kadhaa kutangaza kusitisha safari za ndege za muundo kama huo, zikiwa ni pamoja na China, Uingereza na Ethiopia.

**Jana, maombolezo yaliendelea huku risala za rambirambi zikiendelea kutolewa kwa jamaa za watu 157 waliopoteza maisha.**

Mashirika matatu ya ndege nchini Marekani, Southwest Airlines, American Airlines na United Airlines yamesema ndege hizo za 737 Max zitaendelea na safari, ingawa baadhi ya abiria waliandika ujumbe mbalimbali kupitia mitandao ya kijamii, wakielezea hofu yao na kuuliza kama ndege hizo zinaweza kubadilishwa.

Hali hiyo imejitokeza siku ambayo mamlaka ya usafiri wa angani ya Umoja wa Ulaya ilitangaza marufuku ya ndege hizo katika anga za nchi wanachama wa muungano huo.

Jana, maombolezo yaliendelea huku risala za rambirambi zikiendelea kutolewa kwa jamaa za watu 157 waliopoteza maisha wakati ndege ya shirika la Ethiopia ilipoanguka karibu na mji wa Addis Ababa siku ya Jumapili.

Waathirika hao ni kutoka nchi tofauti 35 ikiwa ni pamoja na wafanyakazi 22 wa UN waliokuwa wakielekea Nairobi kwa mkutano mkuu wa mazingira (UNEA), bendera kwenye ofisi za umoja huo zilipepea nusu mlingoti. **VOA**



Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May, ambaye amekuwa mstari wa mbele kutaka Uingereza kujiondoa kwenye Umoja wa Ulaya (EU). **PICHA: ALLIANCE**

# Ripoti yamtaja Nkurunziza mkandamizaji

**BUJUMBULA,** Burundi

RIPOTI ya jopo la Tume ya Uchunguzi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Burundi, imeeleza kuwa Serikali ya Rais Pierre Nkurunziza imekuwa kandamizi kwa wananchi wa nchi hiyo.

Tume hiyo ya watu watatu inasema hali hiyo si ishara nzuri wakati nchi hiyo ikielekea kwenye uchaguzi mkuu mwaka ujao.

Ripoti hiyo iliwasilishwa kwa Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu wiki hii mjini Geneva.

Jopo hilo limeelezea kusikitishwa na hatua ya Burundi ya hivi karibuni kufungwa kwa ofisi ya UN ya haki za binadamu baada ya kuwapo nchini humo kwa takriban miaka 23.

Tume hiyo ya uchunguzi ni taasisi pekee ya kimataifa ambayo inafuatilia hali ya haki za binadamu nchini Burundi.

Ripoti hiyo inaelezea kwamba, Burundi imeziambia taasisi zote zisizo za kiserikali ambazo ni za kigeni kujiandikisha tena na kuwasilisha orodha ya wafanyakazi wake na pia kutaja ukabila wao.

Tukio hilo limetokea ili kuona kama wanatekeleza mfumo wa mgao mpya uliowekwa kutaka asilimia 60 wawe wa kabila la Hutu na asilimia 40 wawe Watutsi, pia kuangalia kama wanatekeleza kiwango cha chini cha kuwa na wanawake asilimia 30.

Mjumbe mmoja wa tume hiyo, Francoise Hampson, alisema baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali yametangaza kuondoka Burundi badala ya kutekeleza masharti hayo ambayo wanasema ni kinyume na tathmini zao.

"Kuendelea kusinyaa kwa mwanya wa kidemokrasia pia kunaathiri mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi, watetezi wa haki za binadamu, na vyombo huru vya habari nchini Burundi. Hili linatia wasiwasi zaidi hasa ukizingatia kuwa uchaguzi mkuu utafanyika mwaka 2020," alisema Hampson.

Wajumbe wa tume hiyo walisema mzozo wa kisiasa ambao ulizuka nchini Burundi mwaka 2015, wakati Nkurunziza alipotangaza kuwania awamu ya tatu ya uongozi haujasuluhishwa bado.

Wajumbe hao wanahofia suala hilo litakuwa na athari kubwa sana mwaka 2020 na kusema wamepata habari kwamba wanachama wa upinzani wanatishiwa, kunyanyaswa, kukamatwa au hata kupotea.

Balozi wa Burundi kwenye Umoja wa Mataifa huko Geneva, Renovat Tabu, aliwashutumu wanachama wa tume hiyo akiwaita mamluki ambao ni nyenzo ya upinzani nchini humo.

Hata hivyo, Balozi Tabu alipuuza ripoti hiyo kwa kusema kuwa imejaa uongo, kashfa, matusi na taarifa za kisiasa.

Mwisho wa malumbano, Rais wa Baraza la Haki za Binadamu alimkemea Balozi Tabu, na kumtaka asitishe kufanya mashambulizi binafsi na azungumze kwa heshima. **VOA**

# Kairuki afunguka vipaumbele uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amesema vipaumbele muhimu katika uwekezaji nchini ni uchumi wa viwanda hasa kilimo, viwanda vya nguo na ujenzi wa miundombinu.

Kairuki (pichani) alisema hayo ofisini kwake jijini hapa, alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, Sarah Cooke.



Lengo la mazungumzo hayo ilikuwa ni kujadili maeneo muhimu yanayohusu masuala ya uwekezaji na kwamba pamoja na vipaumbele vya kiuchumi, pia alisema maeneo mengine ni elimu na afya.

"Ninafarijika kwa ujio wako na ni ishara nzuri ya uhusiano mzuri uliopo baina ya nchi hizi mbili. Naamini mazungumzo yetu yatasaidia katika fursa za uwekezaji hasa kwa namna Uingereza ilivyochangia kwenye maeneo muhimu nchini ikiwamo elimu," alisema Kairuki

Aliongeza kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji kwa kuzingatia mchango unaotokana na wawekezaji hasa katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo nchini.

Alisema kuwapo kwa Idara ya Uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu ni hatua muhimu kwa kuwa itasaidia kuongeza nguvu ya ufuatiliaji na utekelezaji wa masuala hayo na kuendelea kuleta mabadiliko katika kutatua changamoto zilizozikabili sekta hiyo.

Kairuki alimshukuru balozi huyo kwa hatua ya mazungumzo yenye tija pamoja na kuendelea kuunga mkono Tanzania na kuwataka kuendeleza urafiki huo katika maeneo aliyoyaainisha.

Naye Balozi Cooke aliipongeza serikali ya Tanzania kwa kuwa na sera zinazovutia wawekezaji pamoja na mabadiliko yanayofanywa kuwavutia wawekezaji nchini ikiwamo ulipaji wa kodi.

"Tunaelewa kuwa serikali inafanya jitihada kubwa katika kuboresha mazingira ya biashara ikiwa ni pamoja na mazingira ya ulipaji wa kodi. Tunaahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuwa na mchango katika maendeleo ya nchi na kuimarisha uhusiano uliopo," alisema Cooke.

# CRJE (EA): Tumejizatiti kujenga uhusiano

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya CRJE(EA) Ltd imesema imejizatiti kujenga uhusiano wa manufaa kwa jamii na serikali pamoja na kutekeleza miradi kwa viwango vinavyokubalika kimataifa.

Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Henry Kasapira, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipotoa taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyofanywa na kampuni hiyo kwenye maeneo mbalimbali nchini Tanzania.

"Tunapotekeleza miradi yetu, tunazingatia viwango vya ujenzi kwa kuwa tunalinda hadhi yetu, maana sisi ni miongoni mwa kampuni za ujenzi zenye viwango vya kimataifa vya nyota tano, tukiwa na leseni daraja la kwanza katika ujenzi wa majengo na barabara," Kasapira alisema.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa miradi yao ya ujenzi unazingatia mazingira ya eneo husika, akitolea mfano Zanzibar ambayo ni kisiwa, hivyo majengo yake huzingatia viwango vinavyozingatiwa kimataifa kujenga kisiwani.

Alisema katika miradi yote waliyoitekeleza, ikiwamo ya ujenzi wa shule na majengo ya The Residence Zanzibar, Park Hyatt Hotel Zanzibar na The Melia Hotel Zanzibar, wamepewa vyeti vya uthibitisho na wahandisi washauri.

Kasapira alisema kampuni hiyo licha ya kuwa ya kibiashara, imejikita katika kuhakikisha inafanya kazi zake kwa kuzingatia viwango, ili kufanikisha lengo la serikali la kuwa na miundombinu na majengo imara kwa maendeleo ya sasa na vizazi vijavyo.

"Katika juhudi za kuimarisha uhusiano wetu na serikali au jamii, pia kulingana na uwezo wetu tumekuwa tukijitokeza kushiriki kutatua shida zinazotokana na majanga au ajali zinazozuka ghafla, nasi tunatoa misaada yetu," Kasapira alisema huku akizitolea mfano ajali za Mv Spice Islander na msaada wao kwa taasisi ya mwanaharakati Bibi Siti Bint Saad.


**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**MAGDALENA PETER CHUWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 241 DCF TOYOTA RACTIS.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/0358/2019.**

115111902



**KUPOTEA KWA CHETI**



**Mark A. Mwakatobe** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0418.0169** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Lutengano .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: OB/RB/2462/2019**

115112902



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

13-03-2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe **14/03/2019** kampuni ya **JP TRADERS LTD** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa.
    1. **Kutoka DODOMA** kuelekea **ITIGI** kupitia **MANYONI** gari hilo lenye namba za usajili: **T 813 CLW / T 198 DCQ.**
    2. **Kutoka DODOMA** kuelekea **DAR ES SALAAM** kupitia **VIGWAZA** gari hilo lenye namba za usajili: **T 813 CLW / T** 198 DCQ.
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 23.00 |
| **Upana** | - | mita | 3.00 |
| **Kimo** | - | mita | 5.20 |

Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115115602



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**Said Juma Amer** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba T327 AQYaina ya HONDA Yenye chasis namba **RD11327478,** engine namba **D2081921534.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/1519/2019**

115113702



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: **MJINI MOROGORO**
Usimamizi wa Mirathi **No. 68/2019**
Ombi la **STEPHEN K. MPEKA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **SUZANA SAMWEL**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 10/4/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 8/3/2019

115113102



**CHETI KIMEPOTEA**



**TITUS W.M. LUHENDE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0345/0584** kilichotolewa na **USAGARA SEKONDARI** mwaka 1997.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: AR/RB/9809/06.**

115112502



**CHETI KIMEPOTEA**



**YUSUF JAMA IBRAHIM** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **CS-15021874** kilichotolewa na **GOOD SAMARITAN ENG MEDIUM SCHOOL** mwaka 2015.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: CD/IR/RB/1557/2019.**

115114202



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 12/03/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA** tarehe **15/03/2019** kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **KITUMBEINI** kuelekea **NDURUMA** gari hilo lenye namba za usajili: T741 CPB
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - | mita 4.6 |
| Upana | – | mita 3.0 |
| Kimo | – | mita 17 |

3. Njia itakayotumika **KITUMBEINE** hadi **NDURUMA** kupitia **OLD MOSHI ROAD** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115114102



**CHETI KIMEPOTEA**



**TRESPHORY KISAKALI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **P0443/0560** kilichotolewa na META SEKONDARI mwaka 2014.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**NJ/RB/1367/2019.**

115112402

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NAFASI ZA KAZI

**WAFANYAKAZI WA HOTELINI**, Wanatakiwa wafanyakazi wa Usafi, Wahudumu, Wapishi na Meneja. Bagamoyo mjini, wawe na vyeti na uwezo wa kuongea Kingereza. Kwa Mawasiliano piga namba: 023-2440004/0657 233970/0768 296667

**MIRADI ITAKUPATIA PESA NA AJIRA:** Learn DESIGNING project proposals ,Find DONORS, Establish NGO .1784505108 / 0769505108 / 0716581562.

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*

## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AK TRANSPORTERS LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T **354 BZK SCANIA.** Chassis namba 05141481.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KGD/RB/10070/2018.**

215115402

### KUPOTEA KWA CHETI




**Hoja Faida** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye index namba **S2324-0097** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Mbugani .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: IMC/UK/MDF/VOL.01/2018**

115114802

### KUPOTEA KWA CHETI



**Claudian Tembe** anatangaza kupotea kwa chati cha kidato cha nne chenye index namba **S0153-0595** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la taifa mwaka 2015, Katika shule ya Sekondari Songea Boys.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: SO/RB/506/019**

115115302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 72…2019**
**Mdai: BONIVENTURE N.MWITA**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: CAROLINA RICHARD GASASE**
**Kwa:**
**CAROLINA RICHARD GASASE**
**DAR-ES-SALAAM**

**Ombi la Mdai:**
**BONIVENTURE N.MWITA**
Madai ya: **PESA SHILINGI 2,888,100/= (MILLION MBILI LAKI NANE ELF THEMANINI NA NANE NA MIA MOJA TU).**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi 03 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 12 mwezi 03 mwaka 2019

115113902

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA Mjini
Usimamizi wa mirathi No. 98/2015

Ombi la **HAMIDA I. MANDARI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ISSA MRISHO MANDARI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 20/3/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 13/03/2019

115114002

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Aderina Thomas Bukuku** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba MC 899 BTD aina ya BAJAJ (BOXER) Yenye chasis namba **MD2A21BYOHVVD50118**, engine namba PF2WHD37366.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/1519/2019**

115113502

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Awadhi Ramadhan Ismail** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba T195 DGS aina ya TOYOTA (RACTIS). Yenye chasis namba NCP1000052279, engine namba INZ1768205.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/1519/2019**

115113602

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Christopher Kalokola Christopher** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba T215 DDG aina ya TOYOTA (ALTEZA). Yenye chasis namba GXE100105303,engine namba IG6978263.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/1519/2019**

115113802

### KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI

**ABONIKE ANATORY LAURIAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki iliyokuwa na namba ya usajili **MC 978 BRV** na chasis namba **MD2A21BY8HWA56149** na injini namba **PFZWHA10668.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:
**IR/TR/RB/905/19**

115113202

### CHETI KIMEPOTEA



**BOAZ YONA** anatangaza kupotelewa na cheti cha **UALIMU DARAJA C** chenye namba **KG/6/64** kilichotolewa na KATA YA SIMBO WILAYA KIGOMA VIJIJINI mwaka 1983.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KGT/RB/1522/19.**

115111202

### VYETI VIMEPOTEA



**LUGANO JAMES UISSO** anatangaza kupotelewa na Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1071/0105** kilichotolewa na ST. MATTHEW'S SEKONDARI mwaka 2007. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0534/0572** kilichotolewa na ST. ANTHONY SEKONDARI mwaka 2011.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**BAG/RB/455/2019.**

115112102

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika mahakama ya
Mwanzo DODOMA MJINI.
Usimamizi wa Mirathi NA. 17/2019.
Ombi la **FAUSTINA MKAMA** kuteuliwa
Msimamizi wa Mirathi Marehemu **MOHAMED RWEMAHO MKAMA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/3/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tahehe 12/3/2019

115112602

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AMANI RUBENI SARIA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 743 DPF.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**CID/TR/RB/0357/2019.**

115112002

### KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI

**FAI LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili T 345 CDV, T 881 BCA, T 935 DDG, T 595 CCG, T 487 DCD, T 262 DAU aina ya SCANIA.

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KJN/OB/RB/2019.**

115111802

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC 537 BLH. Chassis namba **MD2A21BZ5GWE91136.** Engine namba. **PFZWGE89591.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/401/2019.**

215112202

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# HAZARD AZUA HOFU YA KUONDOKA CHELSEA

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa Chelsea wameingiwa na "hofu" kuwa huenda Eden Hazard anaweza kuiacha klabu hiyo mwishoni mwa msimu, wakati huu Real Madrid ikiripotiwa kuvutiwa naye, kwa mujibu wa mchezaji mwenza, Emerson Palmieri.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, Hazard amekuwa katika kiwango bora msimu huu akiwa na 'Blues' hao, na tayari ameshatupia mabao 13 na kutengeneza mengine 11 kwenye mechi za Ligi Kuu.

Kwa muda mrefu Hazard amekuwa akihusishwa na kujiunga na Madrid na kurejea kwa Zinedine Zidane kama kocha mkuu kumeongeza tetesi za nyota huyo kujiunga na klabu hiyo wakati huu msimu ukielekea ukingoni.

Mshambuliaji huyo amebakiza zaidi ya mwaka mmoja katika mkataba wake na Chelsea na hivi karibuni alidai mawazo yake ni kuhusu utakapokuwapo mustakabali wake wa baadaye.

Ingawa ameonyesha dalili kidogo za kuondoka, amesifu staili ya uchezaji anayotumia kocha Maurizio Sarri wakati pia akidai angependa kuichezea Madrid, Emerson anaamini kabisa Hazard atabaki Stamford Bridge.

# *Ronaldo: Mfalme wa mtoano Uefa*

**TURIN,** Italia

MABAO matatu ['hat-trick'] aliyofunga Cristiano Ronaldo dhidi ya Atletico Madrid yameonyesha ni kwa nini ni mfalme wa mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ronaldo alifunga mabao matatu wakati Juventus ikishinda 3-0 kwenye mechi iliyopigwa Turin juzi na kuwa timu ya nne pekee kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kuweza kusonga mbele katika hatua hiyo baada ya kupoteza kwa mabao 2-0 katika mkondo wa kwanza. Ni hatua nzuri kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 kwa kuwa mara nyingine tena ameweza kuwa mbele dhidi ya wapinzani wao wa zamani kutoka Jiji la Hispania.

Pamoja na kuisaidia Juventus kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ronaldo ameweka historia nyingine.

Baada ya kufunga mawili kwa kichwa, alitupia kwa mkwaju wa penalti dakika za mwisho na kukamilisha hat-trick - ambayo ni ya nane kwake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambayo inamfanya kumfikia Lionel Messi.

Na wakati linapokuja suala la mabao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano, hata Messi hawezi kumkaribia Mreno huyo.

Mabao hayo yalimfanya kuongeza idadi yake ya ufungaji kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano na kufikia 63 ukilinganisha na 40 ya Messi kwenye hatua hiyo.


## SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

TANZANIA BUREAU OF STANDARDS

### TAARIFA KWA UMMA NA WAZALISHAJI WA BIDHAA

**Shirika la Viwango Tanzania** linapenda kuufahamishwa umma na wazalishaji wote kuwa mwaka 2017 lilianzisha utaratibu wa kuweka alama ya kielektroni kwenye bidhaa zilizothibitishwa ubora wake na TBS. Alama hiyo inamwezesha mteja kutambua aina ya bidhaa muda wake wa matumizi na mzalishaji wa bidhaa husika, kupitia simu ya mkononi.

Utaratibu huu wa alama ya kielektroniki ulianzishwa kwa majaribio na kampuni kadhaa yanayozalisha bidhaa mbalimbali yaliruhusiwa kuweka alama hiyo ya kielektroniki.

Hata hivyo, hivi karibuni kampuni ya SCANCODE imekuwa ikisambaza kalenda za mwaka 2019 zinazoeleza kuwa ina ushirikiano na TBS katika uwekaji wa alama ya ubora ya kieletroniki jambo ambalo si kweli kwa sababu alama hiyo ya kielektroniki kwa sasa imesitishwa kutumiwa na wazalishaji mpaka hapo taratibu za manunuzi za kumpata mzabuni atakayefanya kazi hiyo zitakapokamilika kwa mujibu wa sheria ya manunuzi 2012

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:-**

**Mkurugenzi Mkuu**
**Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**
**S.L.P. 9524**
**Dar es Salaam**
**Simu: +255-22-2450206**
**Hotline: +0800110827**
**Barua pepe: info@tbs.go.tz**
**Tovuti: www.tbs.go.tz**

215114702



## SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

TANZANIA BUREAU OF STANDARDS

### SEMINA KWA WAKALA WA FORODHA NA WAAGIZAJI WA BIDHAA MBALIMBALI KATIKA BANDARI YA TANGA NA MPAKA WA HOROHORO

**Shirika la Viwango Tanzania (TBS)** linapenda kuwafahamisha waagizaji wa bidhaa mbalimbali pamoja na mawakala wa forodha wanaotumia bandari ya Tanga na mpaka wa Horohoro kuwa tarehe **2019-03-20** kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi **saa 7:00 mchana katika ukumbi wa Bandari ya Tanga** kutakuwa na semina.

Lengo la semina hii ni kuelimisha matakwa ya viwango, utaratibu wa uingizaji na uthibitishaji wa bidhaa zinazoingia nchini pamoja na changamoto zilizopo kuhusiana na mifumo na taratibu husika.

Kwa taarifa hii waagizaji na mawakala wa forodha wote wanaotumia bandari ya Tanga na mpaka wa Horohoro mnaombwa kuhudhuria semina hii muhimu bila kukosa.

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Shirika la Viwango Tanzania,**
**S L P 9524, Dar es Salaam.**
**Simu: +255 (022) 2450298; Hotline: +0800 110 827**
**Barua pepe: info@tbs.go.tz; Tovuti: www.tbs.go.tz**

**Ofisi ya Kanda ya Kaskazini –Arusha**
**NSSF Mafao House Building,**
**Ghorofa ya 2,**
**S L P 2399, Arusha.**
**Simu: +255 27 2520143**

215114702



# SIMEONE AKUBALI LAWAMA KIPIGO JUVE

**MADRID,** Hispania

Diego Simeone amekubali kubeba lawama kufuatia Juventus kupindua matokeo yao ya mabao 2-0 na kuitoa Atletico Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mabao matatu ['hat-trick'] kutoka kwa Cristiano Ronaldo kuliufanya usiku wa Jumanne kuwa wa kihistoria Turin, ambapo mchezo ulianza wakati Atletico ikishuka uwanjani ikiwa na ushindi wa mabao 2-0 iliyoupata katika mechi ya mkondo wa kwanza wa hatua ya 16-bora jijini Madrid.

Lakini baada ya mechi, Simeone alibeba lawama zote, kwa kuwaambia wanahabari: "Si kuhusu uwajibikaji, kuhusu kazi ama juhudi. Juventus walikuwa wazuri na walistahili kushinda mechi. Walitusukuma nyuma. Lazima umpongeze mpinzani wakati wanapocheza mechi kama hivyo na umefungwa kama hivyo.

"Tulifanya makosa mengi kwa uhakika - lakini ninamaanisha, si wachezaji. Walikuwa wazuri kiufundi na ndiyo maana wameshinda."

Simeone aliongeza: "Sidhani kwamba kilikuwa kiwango chetu kibovu, wala sikuona kukosa kuheshimu. Kirahisi walicheza vizuri na tunapaswa kuwapongeza. Tulicheza vizuri pia kuelekea mapumziko na kutengeneza nafasi nzuri, lakini hatukuweza kufanya vyakutosha katika kipindi cha pili. Hatukuweza kuwabana.

"Nadhani Juve uimara wao mkubwa ni uwezo wa kupenyeza. Hata tulipokwepa upenyezaji wao hatukuwa wazuri wa kutosha katika mipira inayorudi baada ya kuzuiwa.

"Juventus walicheza kama tulivyofanya katika mechi ya mkondo wa kwanza. Tumehaha na walistahili kusonga mbele robo fainali."



# *Zidane ruksa kusajili wote Neymar, Mbappe-Perez*

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez anatumai Zinedine Zidane anaweza kufanikisha usajili wa Kylian Mbappe wakati pia akishindwa kuweka kando uwezekano wa kusajiliwa kwa pamoja yeye na mchezaji mwenza wa Paris Saint-Germain, Neymar.

Madrid inajiandaa kukibadili kikosi chake mwishoni mwa msimu kufuatia kurejea kwa Kocha Mkuu Zidane, ambaye Jumatatu alirithi mikoba ya Santiago Solari baada ya mabingwa hao watetezi mara tatu wa Ulaya kutupwa nje ya michuano hiyo wiki iliyopita.

Miamba hiyo ya La Liga imehaha msimu huu baada ya Cristiano Ronaldo kuondoka na kutua kwa mabingwa wa Serie A, Juventus, wakati huu Madrid ikishika nafasi ya tatu ikiwa pointi 12 nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Barcelona.

Madrid kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa na nyota huyo wa PSG, Mbappe na straika wa zamani wa Barca, Neymar, na tetesi za kusajiliwa kwa wawili hao ziliongezeka baada ya Zidane kurudi Santiago Bernabeu. Wakati wa mkutano wa Zidane na waandishi wa habari, Perez alitania kuwa kocha huyo raia wa Ufaransa anaweza kuwa sehemu ya kufanikisha kumpata Mfaransa mwenzake.

"Zidane ni Mfaransa, labda anaweza kufanya kitu fulani na Mbappe," Perez aliwaambia wanahabari.

Wakati alipoulizwa kuhusu Mbappe, Perez alijibu: "Kwa sasa, wote tunachokitazama ni kumaliza msimu vizuri na kuanza kujiandaa kwa msimu ujao."

Neymar ameendelea kuhusisishwa na Madrid licha ya kuondoka Barca na kujiunga na PSG kwa uhamisho ulioweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 mwaka 2017.

Alipoulizwa ni nani atamchagua kati ya Neymar na Mbappe, Perez alisema: "Wote."

# Lacazette ruksa kuivaa Rennes

**LONDON,** England

ALEXANDRE Lacazette ameruhusiwa kurejea uwanjani wakati Arsenal ikiivaa Rennes leo baada ya klabu hiyo kukata rufaa kuhusu adhabu iliyokuwa ikimkabili kwenye michuano ya Europa League ya kusimamishwa na UEFA.

Lacazette alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja kwa kumpiga kiwiko Aleksandar Filipovic wakati Arsenal ikichezea kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya BATE katika mechi ya mkondo wa kwanza ya hatua ya 32-bora.

Mshambuliaji huyo alifungiwa mechi tatu na alikosa ile ya marudiano pamoja na wakati wakichapwa 3-1 dhidi ya Rennes timu hizo zilipokutana katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa hatua ya 16-bora.

Lakini UEFA ilithibitisha Jumanne kuwa adhabu hiyo imepunguzwa na kuwa mechi mbili na kutokana na kwamba alitumikia kwa kukosa mechi mbili, anaweza kucheza dhidi ya Rennes leo katika Uwanja wa Emirates.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO: NDIYO MAANA JUVE WAMENILETA HAPA

## Aifikia rekodi ya Messi hat-trick Uefa akipiga bao la 124 na kuitupa nje Atletico huku...

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo amesema mabao matatu ['hat-trick'] aliyofunga dhidi ya Atletico Madrid juzi na kuiwezesha Juventus kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ndiyo sababu iliyoifanya klabu hiyo kumleta Turin, Italia.

**Ronaldo ametwaa ubingwa wa michuano hiyo mara nne katika kipindi cha misimu mitano ili yopita akiwa na Real Madrid, lakini alijiunga na Juve kwa ada ya uhamisho iliyoelezwa kuwa euro milioni 112 kuelekea msimu wa 2018-19.**

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno, alifunga bao moja tu katika hatua ya makundi, wakati pia alitolewa kwa kadi nyekundu walipoivaa Valencia, lakini juzi alionyesha ubora wake kwa staili tofauti na kufanikiwa kupindua matokeo kwa kuitoa Atletico Madrid.

Kikosi hicho cha Diego Simeone, Atletico, kilishuka dimbani kikiwa na ushindi wa mabao 2-0 walioupata nyumbani shukrani kwa mabao kutoka kwa mabeki Jose Gimenez na Diego Godin katika mechi ya mkondo wa kwanza, lakini walikutana na nguvu ya kutisha isiyozuilika kutoka kwa Ronaldo.

Federico Bernardeschi alimimina krosi kutoka wingi wa kushoto iliyomkuta Ronaldo ambaye aliruka juu na kuukwamisha mpira nyavuni kwa kichwa akiiandikia Juve bao la kwanza.

Na wakati kasi ya Bernardeschi ilipozimwa kwa kuchezewa ndivyo sivyo na mtokea benchi Angel Correa, Ronaldo alikamilisha mabao matatu na hivyo kufikia rekodi ya hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa huku Atletico ikiaga rasmi.

"Hii ndiyo sababu ya Juve kunileta hapa, kuisaidia katika usiku wa maajabu kama huu," Ronaldo aliiambia Sky Sport Italia baada ya kuitoa Atletico kwa mara ya tano.

"Atleti ukweli ni timu ngumu kukabiliana nayo, lakini tupo imara pia na tumethibitisha tunastahili kusonga mbele. Ni mapema mno kuzungumza kuhusu fainali, hebu tupige hatua moja kwa wakati."

Kwa mabao hayo matatu ya Ronaldo katika Uwanja wa Allianz, ameihakikishia Juve kupindua matokeo ya mabao 2-0 na kusonga mbele kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza.

"Ni vigumu kuwa usiku wa kipekee na umekuwa," Ronaldo alisema. "Na si tu kwa mabao, bali kwa timu na mtazamo wao wa ajabu.

"Haya ni mawazo unayohitaji katika Ligi ya Mabingwa na tupo kwenye njia sahihi."

Kwa mabao hayo matatu, sasa Ronaldo ameifikia rekodi ya hat-trick nane kwenye Ligi ya Mabingwa iliyokuwa ikishikiliwa na Lionel Messi.

Messi alivunja rekodi ya Ronaldo ya hat-trick wakati Barca iliposhinda mabao 4-0 dhidi ya PSV Septemba mwaka jana, lakini nyota huyo wa Juventus Jumanne akamfikia tena.

Ronaldo, 34, amefikisha jumla ya mabao 124 kwenye mechi 160 alizocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi sasa.

## ZISIKUPITE

### RAMOS, BENZEMA KIKWAZO JOSE

BEKI Mhispania Sergio Ramos na mshambuliaji Mfaransa Karim, wapiga kura ya veto kupinga uwezekano wa Mourinho kurejea kuinoa Real Madrid. Zinedine Zidane aliteuliwa tena kuinoa klabu hiyo ikiwa ni miezi 10 tu tangu aachie ngazi hapo Bernabeu. ***(Sport)***

### SANCHO, COUTINHO KUTUA UTD

MANCHESTER United itafunga safari majira ya joto kwenda kumsajili winga wa Borussia Dortmund, Muingereza Jadon Sancho, 18. Klabu hiyo ya England pia imewasiliana na Barcelona kuhusu uwezekano wa kumsajili Kiungo Mbrazil Philippe Coutinho, 28. ***(Independent)***

### LEWANDOWSKI, BAYERN KUTETA

BAYERN Munich itafanya mazungumzo na straika Mpoland Robert Lewandowski kuhusu kuongeza mkataba. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, amekuwa akihusishwa na Real Madrid. ***(Goal)***

### AVUTIA PUMZI MABEKI

KOCHA wa muda wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer anajiandaa kuwapa nafasi mabeki kuthibitisha ubora wao wenyewe kwa kushikilia kwanza kitita cha pauni milioni 80 alichopewa kwa ajili ya kusajili mabeki wa kati majira haya ya joto. ***(Sun)***

### YAKUBALI KWA HAZARD REAL

CHELSEA inatambua haina cha kufanya katika kumzuia straika Mbelgiji Eden Hazard kuondoka Real Madrid. 'Blues' wanatarajiwa wanaweza kuhitaji tariban pauni milioni 100 ili kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(ESPN)***

### RANIERI AMTAKA DRINKWATER

CLAUDIO Ranieri anataka kufanya tena kazi na kiungo wa Chelsea, Danny Drinkwater. Baada tu ya kuteuliwa kuinoa Roma, Ranieri amejadili na mkurugenzi kumsajili nyota huyo waliyefanya naye kazi Leicester City. ***(Tribal)***

### WEST HAM KUMRUDIA GOMEZ

WEST Ham itarudi tena kwa mshambuliaji wa Celta Vigo, Maxi Gomez, 22, baada ya mpango wao wa kumsajili Mruguay huyo Januari kukwama. ***(Mirror)***

### KARIUS BADO KUBAKI BESIKTAS

KIPA wa Liverpool, Loris Karius, 25, ataendelea kubaki Besiktas kwa mkopo licha ya kocha wa klabu hiyo kusema "kuna tatizo" kwa mlinda mlango huyo. ***(ESPN)***

### PALACE KUMFUATA DIAME

CRYSTAL Palace na Brighton ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa kumsajili kiungo wa Newcastle United, Mfaransa Mo Diame, 31. ***(Star)***

### ARSENAL, MADRID VITANI

ARSENAL imejiunga katika mbio za kumsajili beki wa Ajax, Nicolas Tagliafico, 24. Kikosi hicho cha Unai Emery sasa kitashindania saini ya beki huyo na Real Madrid, Atletico Madrid, Man Utd na Liverpool. ***(Footy Cosmos)***

### RICE KUONA MWEZI ENGLAND

KIUNGO wa West Ham, Declan Rice anatarajiwa kuitwa kuichezea England kwa mara ya kwanza wakati huu ikielekea kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Jamhuri ya Czech na Montenegro. ***(Guardian)***

HABARI MICHEZO

# ZFA yajipanga kuwanoa waandishi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Soka Zanzibar (ZFA), kinatarajia kutoa mafunzo kwa waandishi wa habari za michezo ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi za kuripoti mechi na matukio mbalimbali wanapokuwa uwanjani, imeelezwa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya ZFA, Hussein Ahmada, alisema mafunzo hayo yatakuwa ya siku moja na yanatarajiwa kufanyika Machi 26, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Uwanja wa Amaan na tayari maandalizi ya awali ya mafunzo hayo yameshaanza.

Ahmada alisema mkufunzi wa mafunzo hayo anatarajiwa kuwa mwandishi wa habari wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Aisha Nakato, ambaye anafanya kazi katika Kituo cha Televisheni cha Awowo (TV Awowo) cha Uganda.

Alisema katika mafunzo hayo kutakuwa na vipengele mbalimbali ikiwamo juu ya kuripoti habari za michezo kwa waandishi wa magazeti, TV na wa redio, pamoja na upigaji picha hususan katika mechi za kimataifa.

Aliongeza kuwa ZFA imeamua kuandaa mafunzo hayo ili kuwaongezea elimu wadau hao wa habari kwa ajili ya kusaidia kuendeleza mbele gurudumu la soka Zanzibar.

"Mafunzo hayo yatakuwa bure kabisa, hivyo ni waandishi wa habari wote wanaombwa kufika Ofisi za ZFA ili kuthibitisha ushiriki wao katika mafunzo hayo ambayo yana umuhimu katika kuendeleza taaluma zao," alisema Ahmada.

Alisema pia ZFA imepanga kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wadau wake ili kuhakikisha malengo ya kukuza na kulitangaza soka katika visiwa hivyo yanatimia.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 27 | 21 | 4 | 2 | 45 | 18 | 67 |
| 2. Azam | 27 | 16 | 8 | 3 | 42 | 18 | 56 |
| 3. Simba | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4. Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 5. Mtibwa Sugar | 28 | 12 | 5 | 11 | 29 | 21 | 41 |
| 6. Lipuli | 30 | 9 | 12 | 9 | 24 | 26 | 39 |
| 7. Coastal Union | 29 | 8 | 13 | 8 | 27 | 30 | 37 |
| 8. Mbao | 29 | 9 | 10 | 10 | 19 | 26 | 37 |
| 9. Mwadui | 30 | 10 | 6 | 14 | 34 | 37 | 36 |
| 10.JKT Tanzania | 30 | 8 | 12 | 10 | 18 | 24 | 36 |
| 11. Alliance | 29 | 9 | 9 | 11 | 23 | 30 | 36 |
| 12. Mbeya City | 28 | 9 | 7 | 12 | 28 | 32 | 34 |
| 13. Ruvu Shooting | 29 | 8 | 10 | 11 | 27 | 35 | 34 |
| 14. Kagera Sugar | 28 | 7 | 12 | 9 | 21 | 26 | 33 |
| 15. Stand Utd | 30 | 9 | 6 | 15 | 27 | 39 | 33 |
| 16. Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 17. TZ Prisons | 28 | 7 | 11 | 10 | 20 | 24 | 32 |
| 18. Singida Utd | 28 | 8 | 8 | 12 | 20 | 27 | 32 |
| 19. Biashara Utd | 28 | 6 | 9 | 13 | 20 | 29 | 27 |
| 20. African Lyon | 29 | 4 | 10 | 15 | 18 | 36 | 22 |

# SINGIDA UNITED: UKATA UNATUYUMBISHA BARA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kuendelea kupoteza pointi Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Singida United umesema tatizo kubwa linaloifanya klabu hiyo ifanye vibaya ni ukosefu wa fedha za uendeshaji.

**Kauli hiyo ilitolewa juzi jioni baada ya Singida United kufungwa bao 1-0 na wenyeji Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro.**

Singida United yenye pointi 33, imecheza mechi 29 na katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 iko kwenye nafasi ya 17 baada ya kushinda mechezo nane, sare tisa na kufungwa mechi 12.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa Singida United, Festo Sanga, alisema hali hiyo inawafanya wanashindwa kuihudumia vema timu yao na kufanya maandalizi yanayostahili kabla ya kushuka uwanjani.

Sanga alisema kupungua kwa wadhamini ndiko kumechangia klabu yao "kuyumba" na kushindwa kuonyesha makali yake kama ilivyokuwa katika msimu wake wa kwanza iliposhiriki ligi hiyo wakiwa chini ya Rais wa klabu hiyo, Mwigulu Nchemba.

"Ukata unatumaliza, hali mbaya ya kiuchumi tuliyonayo inatumaliza, hatujafilisika lakini tumeyumba, kipato chetu kimepungua," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa pamoja na changamoto hiyo, bado wataendelea kupambana kuhakikisha wanabaki kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na kurejea kwa kocha, Fred Minziro kutaongeza nguvu katika kikosi chao.

Yanga yenye pointi 67 wako kileleni katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kila mwaka ambayo yanaandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).



Sergio Aguero akishangilia baada ya kuifungia Man City bao la pili wakati ikishinda 7-0 dhidi ya Schalke kwenye mechi ya mkondo wa pili ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi. City imesonga mbele kwa jumla ya mabao 10-2. **PICHA: MTANDAO**

# Kocha KVZ atamba kutwaa ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa KVZ, Shekha Khamis, amesema bado malengo yake ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu hayajafutika.

Shekha ambaye timu yake mzunguko wa kwanza iliongoza msimamo wa ligi hiyo kwa muda mrefu, alitoa kauli hiyo juzi jioni baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mwenge.

Alisema anaamini atarejea tena katika nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa ligi hiyo kutokana na kikosi chake kuendelea kuimarika na hatimaye kutimiza malengo yao waliyojiwekea wakati wanaanza msimu.

Kocha huyo aliongeza kuwa soka ni mchezo wa makosa, hivyo kupoteza mechi haina maana kuwa kiwango cha wachezaji wake kimeshuka au kimepoteza matumaini ya kunyakua ubingwa wa ligi hiyo.

Mabao ya KVZ yenye pointi 55 ikiwa nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo, yalifungwa na Ayoub Lipati dakika ya 18 na Abdul Yusuph aliyeiandikia timu yake bao la pili dakika ya 26 wakati bao pekee la Mwenge liliwekwa kimiani na Jumanne Alawi dakika ya 52.

Katika mchezo mwingine wa ligi hiyo, JKU ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Jamhuri, bao hilo pekee likifungwa na Mbarouk Chande wakati kwenye Uwanja wa Mao, Mafunzo iliichapa Mbuyuni mabao 3-0 huku Mlandege ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Selem View katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

Polisi walichapwa mabao 2-0 na Chipukizi katika mechi nyingine iliyochezwa kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

Kwa matokea hayo timu ya KVZ imepanda nafasi moja ambapo sasa ipo nafasi ya pili ikitokea nafasi ya tatu ambapo ina alama 55, huku timu ya Mwenge yenyewe ikiwa katika mstari hatari wa kushuka daraja ambapo ipo nafasi ya 14 na ikiwa na alama 20.

# Michezo

Alhamisi Machi 14, 2019

Nipashe



Lacazette ruksa kuivaa Rennes

HABARI UK. 29

UWANJA MPYA...



Rais John Magufuli akizungumza jambo kuhusu ujenzi wa uwanja wa mpya wa soka utakaojengwa jijini Dodoma ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua watazamaji zaidi ya 85,000, huku Balozi wa Morocco hapa nchini, Abdelilah Benryane (wanne kushoto), pamoja na Kiongozi wa Ujumbe kutoka nchini Morocco, Balozi Mohamed Methqal (watatu kushoto), na ujumbe huo wakimsikiliza walipofika Ikulu jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya mazungumzo. **PICHA: IKULU**

## Ajibu afunguka, Matola awaonya

**Somoe Ng'itu Dar na Friday Simbaya,** Iringa

WAKATI vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ya jijini Dar es Salaam wakitamba wanakwenda Iringa kwa kazi moja ya kuchukua pointi tatu ingawa wanafahamu wazi mchezo wao dhidi Lipuli FC hautakuwa mwepesi, kocha wa wenyeji wao hao, Selemani Matola amewataka mashabiki kujitokeza kwa wingi katika Uwanja wa CCM Samora Jumapili kushuhudia wakifanya kweli.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha wa Yanga, Ibrahim Ajibu, alisema kuwa timu yao ina "kiu" ya kuchukua ubingwa wa ligi hiyo ili waweze kutimiza malengo yao na wanafahamu hawatakiwi kupoteza tena pointi.

Ajibu alisema kuwa kila mchezaji wa Yanga ambaye atapata nafasi ya kucheza, anafahamu mipango iliyowekwa na benchi la ufundi, klabu na timu yote kwamba wanahitaji matokeo ya ushindi na si kitu kingine.

"Tunajua walioko nyuma watatukimbiza, hakuna ambaye anafurahi kuona tunaongoza ligi kwa muda mrefu, ingawa baadhi ya timu kama Simba zimecheza mechi chache, hiyo hatuiangalii, tunachoangalia ni kufanya vizuri katika kila mechi tutakayocheza," alisema Ajibu.

Mshambuliaji huyo aliongeza kuwa kila mchezaji anatakiwa kujituma katika dakika zote atakazokuwa uwanjani na kwao neno kukata tamaa halipo.

Naye Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa kikosi cha timu hiyo kinatarajia kuelekea Iringa leo, huku wakiwa na tahadhari ya kuwavaa Lipuli.

Lakini wenyeji wao, Lipuli wametamba kuwa wamejipanga kuibuka na ushindi katika mchezo huo dhidi ya Yanga na hiyo ni kauli ya Kocha wa timu hiyo, Matola.

"Sisi benchi la ufundi tumelifanyia kazi jambo hilo na sasa tunajipanga kuhakikisha tunaibuka na ushindi katika uwanja wetu wa nyumbani," alisema Matola.

# Wawa awatuliza Simba

**Na Somoe Ng'itu**

## Asema yupo imara kama 'chuma cha pua' kuiva AS Vita Taifa Jumamosi, hesabu sasa...

BEKI wa kati tegemeo wa Simba, Pascal Wawa amewaondoa hofu mashabiki wa klabu hiyo kwa kusema yuko "fiti" na anaweza kuiongoza safu ya ulinzi ya timu hiyo katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Wawa aliumia kifundo cha mguu ('enka') katika mechi iliyopita dhidi ya JS Saoura iliyochezwa Jumamosi iliyopita mjini Bechar, Algeria, ambapo wawakilishi hao pekee wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati waliobakia kwenye michuano hiyo walipokubali kichapo cha mabao 2-0.

Akizungumza na gazeti hili, Wawa alisema kuwa anaendelea vizuri na jana asubuhi alifanya mazoezi na wachezaji wenzake kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mchezo huo utakaochezeshwa na waamuzi kutoka Morocco kuanzia saa 1:00 usiku.

**Wawa alisema kuwa anaamini kikosi cha Simba kitapambana kwa sababu kinataka kuwafurahisha mashabiki wake na vilevile kuweka rekodi nzuri kwao.**

"Niko vizuri sasa, niliumia katika mechi iliyopita kule Algeria, lakini sasa ninaendelea vizuri na nitacheza mechi ya Jumamosi." Wawa, beki wa zamani wa Azam ambaye ni raia wa Ivory Coast aliliambia Nipashe kwa kifupi jana mchana.

Mbali na Wawa, Daktari wa Simba, Yassin Gembe, alimtaja mchezaji mwingine ambaye ni majeruhi lakini anaendelea vema ni kiungo Mnyarwanda, Haruna Niyonzima.

"Wawa na Haruna wameumia enka hii ilisababishwa na nyasi bandia zilizoko kwenye Uwanja tuliochezea mechi dhidi ya JS Saoura, lakini kuna maendeleo makubwa katika majeraha yao," alisema daktari huyo.

Simba ambao pia ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaburuza mkia katika kundi hilo wakiwa na pointi sita ambazo walizipata baada ya kuwafunga JS Saoura mabao 3-0 katika mchezo wa kwanza na ilipowakaribisha Al Ahly pia ilipata ushindi wa bao 1-0.

Tayari timu hiyo inayofundishwa na Mbelgiji, Patrick Aussems na Mtanzania, Dennis Kitambi, inahitaji ushindi tu ili iweze kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano hayo ya kimataifa yanayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >